

## Atiwa mbaroni kwa tuhuma kuua 'hausigeli'

UKURASA 3

## Polisi waanika kilichojificha matukio ya wizi wa watoto

UKURASA 2





## Watozwa nauli kubwa kinyume cha taratibu, LATRA yacharuka

UKURASA 5



## KLOPP AKUNWA NA SLOT

UKURASA 22


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Agosti 25, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0581779




Msemaji wa Jeshi la Polisi, DCP David Misime

# Miili ya waliotekwa, kutoweka yapatikana imenyofolewa viungo

**WATUHUMIWA** wakamatwa, wawapeleka polisi walikoifukia... Uk. 4

UKURASA WA 24

## YANGA KUONGEZA NGUVU KIUNGO, BEKI WA KATI

IMEBAINIKA kuwa klabu ya Yanga ina mpango wa kusajili kiungo mkabaji kwa ajili ya kusaidiana na Khalid Aucho na beki wa kati...

## Jalada la 'Afande' ubakaji wa 'Binti wa Yombo' latua kwa DPP

UKURASA 2



## Samia ampa simba jina la Tundu Lissu, azindua utalii wa kasa Z'bar

UKURASA 2

Rais Samia Suluhu Hassan akiangalia uzuri wa pango pamoja na kasa ambao wamekuwa kivutio cha watalii, baada ya kuzindua Utalii wa Kasa katika Pango la Salaam, Kizimkazi Dimbani, Mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

**MICHEZO** SIMBA YATAMBA KUENDELEZA DOZI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Jalada la 'Afande' vijana kubaka 'Binti wa Yombo' latua kwa DPP

**Na Romana Mallya**

JALADA kuhusu tuhuma za anayedaiwa afande wa jeshi kutuma vijana kubaka na kulawiti binti anayedaiwa mkazi wa Yombo Dovya, mkoani Dar es Salaam, limetua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP).

Jeshi la Polisi limesema kuwa tayari jalada hilo linalomhusisha Fatuma Kigondo, anayetuhumiwa kutuma vijana hao, liko mikononi mwa DDP kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) David Misime, aliyasema hayo jana wakati akizungumzia kuhusu tukio hilo na matukio mengine ya watu kuuawa baada ya awali kuripotiwa kupotea na kutekwa.

"Jeshi la Polisi linapenda kutoa taarifa kuhusu Ofisa wa Polisi anayetajwa kwa jina la Fatuma Kigondo kwamba, uchunguzi wa kina ulishafanyika ikiwa ni pamoja na kupata maelezo ya watu mbalimbali na maelezo yake na jalada vimepelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka," alisema.

Agosti 4 mwaka huu, katika mitandao ya kijamii, kulisambazwa video ikionesha namna vijana watano wakimfanyia ukatili huo binti huyo huku wakimrekodi.

Katika video hiyo, vijana hao walisikika wakimtuhumu kutembea na mume wa mtu na binti huyo kusikika akiomba msamaha mtu aliyetambulishwa kama afande.

Tayari kuna kesi mahakamani mkoani Dodoma inaendelea dhidi ya watuhumiwa wa ukatili huo huku kukiwa na shinikizo 'afande' anayedaiwa kuwatuma, naye afikishwe mahakamani.

Baadhi ya mawakili pia wamefungua kesi jijini Dodoma dhidi ya Fatuma, wakimhusisha na ukatili huo.

Hata hivyo, kwa sheria za Tanzania, mamlaka ya kuchunguza, kukamata na kushtaki mtu kwa kesi ya jinai yako kwa Jeshi la Polisi na mamlala linazoshirikiana nazo, ikiwamo ofisi ya DPP.

Tukio hilo la binti kutendwa ukatili huo, liliibuliwa na aliyekuwa Meya wa Ubungo, Boniface Jacob wiki mbili zilizopita ambaye aliandika mkasa mzima kwenye ukurasa wake wa X huku akiwatumia nakala, Rais Samia Suluhu Hassan kama Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi Tanzania, Waziri wa Ulinzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Stergomena Tax na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima.

Boniface aliandika: "Binti huyu amebakwa na kulawitiwa akiwa anarekodiwa video tatu tofauti. Askari hao walimrekodi wakiwa wanambaka na kumlawiti, wamesambaza video zake mitandaoni kwa maagizo ya kiongozi wao (afande) ambaye amewatuma kumpatia huyu binti adhabu.

Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16, kosa la kubaka kwa kikundi, adhabu yake ni kifungo cha maisha gerezani, hivyo washtakiwa hao wakithibitika kutenda ukatili huo, watakumbana na adhabu hiyo.



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Mkurugenzi Kampuni ya Unywaji na Uuzaji wa Maziwa nchini, Ahmed Asas wakati wa hafla ya uzinduzi wa utalii wa kasa katika Pango la Salaam (Salaam-Cave), Kizimkazi Dimbani, Mkoa wa Kusini Unguja jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia ampa simba jina la Lissu, azindua utalii wa kasa

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameelekeza simba dume katika Tamasha la Kizimkazi, Mkoa wa Kusini Unguja, visiwani Zanzibar, aitwe Tundu Lissu.

Kwa mujibu wa kiongozi aliyekuwa akitoa maelezo kwa Rais Samia katika tamasha hilo jana, simba huyo ambaye yumo ndani ya banda alimohifadhiwa akiwa anazunguka huku na huko, alisema moja ya tabia za simba huyo anapoona watu huwa hivyo, lakini hana tatizo.

Baada ya maelezo hayo, Rais Samia aliuliza jina la simba huyo na alipoelezwa kwamba hajapatiwa jina, ndipo aliposema aitwe Tundu Lissu.

Rais Samia wakati akifanya ufunguzi wa bwawa la kisasa la kuhifadhia kasa ikiwa ni miongoni mwa matukio katika Tamasha la Kizimkazi kwa mwaka huu, aliwataka wananchi kulitumia kama fursa za kujijenga kiuchumi na kulinda utamaduni wa nchi.

Alisema kuwapo tamasha hilo kunachangia kwa kiasi kikubwa shughuli za uwekezaji pamoja na kupanua mji huo, hivyo ni vyema wananchi kuchangamkia fursa zilizoko.

Alisema kuna fursa nyingi ambazo zinapatikana Kizimkazi hasa zinazohusu sekta ya utalii wa bahari pamoja na mapango ya kale.

Rais Samia alipongeza jitihada kubwa zilizofanywa kwa sekta ya utalii Zanzibar na kueleza kuwa kuna haja ya kutunza mazingira kwa kuhifadhi viumbe vya baharini kama kasa.

Alisema kasa licha kuwa kivutio cha utalii, watapata sehemu ya kuhifadhiwa na baadaye kurejeshwa baharini.

"Niwapongeze kwa jitihada kubwa mlizofanya kwa kubuni jambo hili ambalo kwanza, limetunza mazingira na uhifadhi bora," alisema.

Rais Samia alisema kivutio hicho cha utalii kitaingizwa katika mtandao wa vivutio vya utalii Tanzania ili kuwavutia wageni wengi zaidi.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohmed, alisema mkoa huo una wastani wa vivutio 17, zikiwamo fukwe za bahari, misitu na majengo ya asili.

Alisema wageni wengi wanaokwenda kutalii huko huangalia samaki aina ya pomboo (dolphine) na msikiti wa kale pamoja na kasa.

Alisema kuwapo tamasha hilo la Kizimkazi kumeongeza kivutio cha utalii, pia kutaongeza idadi ya watalii wanaotembelea mkoa huo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijazi, alisema eneo hilo ni muhimu na linatengeneza ajira pamoja na uchumi wa taifa na kuwa mfano wa kutunza mazingira.

***Imeandaliwa na Romana Mallya na Rahma Suleiman**

## Polisi waanika kilichojificha matukio ya wizi wa watoto

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMANDA wa Polisi Mikoa ya Mwanza na Shinyanga wamesema uchunguzi wa muda mrefu umebaini matatizo ya uzazi katika familia ndicho chanzo cha matukio ya wizi wa watoto.

Wamesema hali hiyo ni tofauti na imani potofu zilizojengeka miongoni wa jamii zikihusisha matukio ya watoto kupotea na masuala ya imani za kishirikina pamoja na Uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani.

Kamada wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbrod Mutafungwa, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa ya kumkamata George Mlalo (21), mkazi wa Kisiwa cha Kamasi, wilayani Ukerewe, mkoani humo, kwa tuhuma za wizi wa mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja na kuishi naye.

Alisema sehemu kubwa ya watuhumiwa wanapokamatwa wamekuwa wakitaja kukosa watoto katika ndoa zao na hivyo kutamani kuiba watoto.

"Sababu hii imekuwa ikijitokeza katika matukio tunayokamata wanaume kwa wanawake. Hali hiyo inachangiwa na lawama na migogoro ya kukosa watoto ndani ya ndoa," alisema Kamanda Mutafungwa.

Alisema mtuhumiwa huyo ambaye ni mvuvi, alikamatwa Agosti 16 mwaka huu, saa moja jioni katika Kisiwa cha Ghana, wilayani Ukerewe kwa tuhuma za kumuiba mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja (jina tunalo), mkazi wa Kisesa, wilayani Magu, kwa madai kuwa alimpenda na kuamua kuishi naye.

"Mtoto tumemfanyia uchunguzi na tumebaini kuwa yupo salama, hivyo kumrejesha kwa mama yake Irine Festo (22), na mtuhumiwa anaendelea kuhojiwa na upelelezi ukikamilika atafikishwa mahakamani kujibu tuhuma hizo," alisema Kamanda Mutafungwa.

Katika tukio lingine, Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, amethibitisha kukamatwa kwa Hadija Juma (24), mkazi wa Kijiji cha Sengerema, wilayani Uyui, mkoani Tabora, kwa tuhuma za wizi wa mtoto wa kike. Kamanda Janeth alisema wizi huo uliotokea Agosti 20 mwaka huu, saa 12 jioni, katika Kituo cha Afya Ushetu, wilayani Kahama, mkoani humo.

"Mtuhumiwa tumemhoji na amekiri kutenda kosa na sababu ni zilezile kwamba, amekuwa anaolewa lakini hajafanikiwa kuzaa na hadi sasa amefikisha ndoa ya pili na kuachika. Taratibu za kumfikisha mahakamani zinaendelea," alisema Magomi.

Alisema mtoto huyo alizaliwa Agosti 17 mwaka huu na taarifa za kuibwa zilitolewa polisi Agosti 21 katika Kituo cha Polisi Nyamilangano, Ushetu, ndipo ufuatiliaji ulipoanza na mtuhumiwa kukamatwa Agosti 22 mwaka huu, saa tatu usiku.

*** Imeandaliwa na Marco Maduhu (SHINYANGA) na Vitus Audax (MWANZA)**

HABARI KITAIFA

# Mbaroni tuhuma kuua msichana wa kazi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JACKSON Magoti (30), mkazi wa Michese Tanesco, jijini Dodoma, anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mwanza kwa tuhuma za mauaji ya mfanyakazi wa ndani, Sainethi Kakululu (20), mkazi wa Mtaa wa Ipuli, Mahina, jijini hapa.

Taarifa ya kukamatwa kwa Magoti ilitolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) Wilbrod Mutafungwa wakati anazungumza na waandishi wa habari.

Kamanda Mutafungwa alisema mtuhumiwa huyo alitiwa mbaroni Agosti 16 mwaka huu, saa 5:30 asubuhi jijini Dodoma alikodaiwa kukimbilia baada ya kutekeleza mauaji hayo.

"Mtuhumiwa huyu alikuwa anafanya kazi ya kusafisha bustani ya nyumba ya Jackline Ngowi, ambako pia alikuwa anafanya kazi za ndani Sainethi.

"Uchunguzi wa awali umebaini alitekeleza mauaji hayo ili kutimiza azma ya kuiba mali zilizokuwa ndani ya nyumba ya Ngowi," alidai Kamanda Mutafungwa.

Alisema Magoti anadaiwa kumuua msichana huyo kwa kumkaba shingoni, kisha kupora vitu mbalimbali ndani ya nyumba hiyo alimokuwa anafanyia kazi.

Alisema kuwa baada ya mauaji hayo, Agosti 5 mwaka huu, saa 11:30 jioni, Jeshi la Polisi lilianza kumfuatilia mtuhumiwa na ndipo alipokutwa nyumbani kwao Dodoma.

"Alikutwa na vielelezo mbalimbali alivyopora ikiwamo simu ya marehemu, viatu pamoja na baadhi ya nguo za marehemu," alisema.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Mutafungwa aliwataka wananchi kutoa taarifa za wahalifu na uhalifu haraka pindi wanapoubaini ili kusaidia jeshi hilo kuchukua hatua za haraka.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea na operesheni katika maeneo ya Ziwa Victoria ili kudhibiti wahalifu na uhalifu ziwani huko.

Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16, adhabu ya kuua kwa kukusudia ni kunyongwa hadi kufa, hivyo kijana huyo akithibitika mahakamani kufanya mauaji hayo, atakabiliwa na adhabu hiyo.



Rais wa Hospitali ya Watoto ya Chuo Kikuu cha Nanjing, nchini China, Dk. Mo Xuming, akiwachunguza magonjwa ya moyo baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Msasani, Dar es Salaam jana. Wataalamu wa moyo kutoka nchi hiyo, wameanza uchunguzi wa magonjwa ya moyo ya kuzaliwanayo kwa wanafunzi na wamekwishawafikia wapatao 900 katika shule mbili za Msasani na Hananasifu, mkoani humo. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**.

# Dk. Mwinyi aapisha wateule wake

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameapisha makatibu wakuu wanne aliowateua hivi karibuni.

Hafla ya uapisho huo ilifanyika Ikulu, Zanzibar na kuratibiwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Zena Ahmeid Said.

Walioapishwa ni Dk. Habiba Hassan Omar, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ambaye amechukua nafasi ya aliyekuwa Katibu wa Wizara hiyo, Dk. Mngereza Mzee Miraji aliyeteuliwa kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya. Awali, Dk. Habiba alikuwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya.

Rais Dk. Mwinyi pia amemwapisha Dk. Mngereza Mzee Miraji kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya. Kabla ya nafasi hiyo, Dk. Miraji alikuwa Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

Wengine walioapishwa ni Maryam Juma Abdalla Saadalla kuwa Katibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kabla ya uteuzi huo, Maryam alikuwa Katibu Mkuu (Kazi na Uwezeshaji) katika Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

Rais Dk. Mwinyi pia amemwapisha Khamis Suleiman Mwalim kuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Kabla ya nafasi hiyo, Khamis alikuwa Katibu Mkuu (Uchumi na Uwekezaji) katika Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

Hafla ya uapisho huo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wakiongozwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Sulemain Abdulla, viongozi wa dini pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama.

# Majaliwa: Barabara za vijijini zitaboreshwa kukuza uchumi

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amepanga kuk

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali inaendelea kufungua mtandao wa barabara za vijijini katika Wilaya ya Ruangwa ili ziweze kusaidia wananchi kusafirisha mazao yao.

Majaliwa ambaye pia ni Mbunge wa Ruangwa, alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Namikulo, Kata ya Chunyu, wilayani Ruangwa, mkoani Lindi.

Alizitaja barabara hizo kuwa ni ya kutoka Namkatila, Matambalale A, Matambalale B Namikulo hadi Nangwego, ambayo alisema imekwishafanyiwa tathmini na itaanza kujengwa mkandarasi akipatikana.

"Barabara hii imeshafanyiwa tathmini na michoro iko tayari. Benki ya Dunia (WB) wanatafuta mkandarasi ili ifikapo Januari 2025, kazi ya ujenzi ianze," alisema.

Majaliwa alisema barabara nyingine ni ya kutoka mjini Ruangwa hadi Namichiga yenye urefu wa kilometa 21 ambayo itajengwa kwa kiwango cha lami.

"Hii itajengwa na TANROADS (Wakala wa Barabara Tanzania) kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (WB). Na sera ya sasa hivi, inataka barabara za lami zikipita kwenye vijiji, maeneo hayo yawekwe taa za barabarani ili wananchi waweze kufanya kazi za kujikimu. Tunamshukuru Rais Samia kwa kuleta fedha hizo," alisema.

Kuhusu ujenzi wa barabara za vijijini ambazo si za lami, Majaliwa alisema serikali inaendelea kuziimarisha na kutolea mfano barabara ya kutoka Chikwale-Machang'anja ambayo inapitika bila shida.

Alisema awamu ya pili ya barabara hiyo itatoka Namichiga-Namkonjela -Nambilanje-Nanjalu- Kiperemende hadi Nanjilinji, wilayani Kilwa. Alisema barabara hiyo imelenga kwenda hadi wilaya nyingine ili kupanua wigo wa mawasiliano, bado haijapata fedha.

Akitoa taarifa kuhusu barabara nyingine kwa wakazi wa kijiji cha Namikulo na vijiji jirani vya Kata ya Chunyu, Meneja wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA) Wilaya ya Ruangwa, Mhandisi Mashaka Nalupi, alisema barabara ya kutoka Chunyu-Mihewe yenye urefu wa kilometa sita imetengewa Sh. milioni 150 na itajengwa kiwango cha changarawe.

"Ipo barabara ya kutoka Chunyu-Namikulo ambayo imetengewa Sh. milioni 10 kwa ajili ya kuichonga barabara hiyo na kujenga mifereji, lakini pia kuna barabara ya kutoka Namilema-Matambarale ambayo itajengwa kwa kiwango cha udongo," alisema.

Kuhusu tatizo la maji, Meneja wa Wakala ya Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA) wa Wilaya hiyo, Mhandisi Lawrence Mapunda, alisema wamekwishachimba kisima katika kijiji cha Liuguru chenye uwezo wa kutoa lita 10,500 kwa saa.

"Kisima kilichimbwa tangu Julai, 2024. Tayari tumetenga Sh. bilioni 1.9 na sasa tunatafuta mkandarasi wa kusambaza maji hayo katika vijiji vinne vya Chunyu, Namikulo, Mihewe na Chiundu," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Miili ya waliotekwa, kutoweka yapatikana imenyofolewa viungo

Na Romana Mallya

KUKIWA na hoja kwamba Rais aunde tume kuchunguza matukio ya utekaji watu nchini, miili ya watu watatu walioripotiwa kutekwa au kutoweka kwa nyakati tofauti, imepatikana.

Baadhi ya miili hiyo imekutwa ikiwa imenyofolewa viungo, huku watuhumiwa wakidai kutenda uhalifu huo kwa lengo la kupata utajiri.

Miili ya watu hao watatu imeripotiwa kukutwa katika mikoa mitatu tofauti. Watu hao wanadaiwa kuuawa katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Singida ndani ya mwezi huu.

Kati ya miili hiyo, upo uliokutwa umefukiwa ndani ya chumba chini ya kitanda na mwingine wa anayedaiwa Katibu wa Wazazi Tawi la Maguruwe, Kata ya Tandika, Temeke, uliokutwa umetenganishwa viungo na kufungwa katika viroba.

Mwingine umekutwa umenyofolewa sehemu ya siri kwa madai kuwa wahusika waliagizwa na mganga wa kienyeji kufanya hivyo ili kutajirika.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) David Misime, aliyasema hayo jana alipozungumzia matukio ya watu kutekwa na kutoweka katika mazingira yenye utata na baadaye kukutwa wameuawa.

"Tukio la kwanza ni la kijana Samwaja Saidi (22), mkazi wa Kijiji cha Chalunyangu, mkoani Singida. Alitoweka tangu Agosti 8 mwaka huu, katika mazingira ya kutatanisha na Agosti 23 mwaka huu, mwili wake ulikutwa umefukiwa katika shimo na sehemu za siri zikiwa zimekatwa," alisema.

Naibu Kamishna Misime alisema tukio hilo liliripotiwa katika Kituo cha Polisi Makuro na kufunguliwa jalada la uchunguzi ambao ulianza mara moja.

Alisema katika ufuatiliaji wao, walipata taarifa kutoka kwa kijana mmoja ambaye alieleza kuwa siku ya tukio walikwenda na Said kutazama mpira na wakati wakirejea nyumbani walikutana na vijana wawili.

"Hao vijana wawili wakamwambia Saidi waende kunywa pombe. Tangu hapo hakuonekana tena na ndipo ndugu walipotoa taarifa polisi.

"Baada ya vijana hao wawili kukamatwa, walikiri siku hiyo walikwenda kunywa pombe na Saidi na wakati wanarejea nyumbani, walimnyonga na kumkata sehemu za siri na kufukia mwili katika shimo.

"Sababu za kufanya hivyo walieleza kwamba, walielezwa na mganga wa kienyeji wakiweza kupata sehemu za siri watakuwa matajiri," alisema.

Naibu Kamishna Misime alisema vijana hao walisema wako tayari kutoa ushirikiano walikofukia mwili huo.



Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime

Alisema kuwa baada ya taratibu kufuatwa, Agosti 24 mwaka huu, vijana hao walikwenda kuonesha eneo uliko mwili huo na ulitambuliwa kuwa ni wa Saidi.

"Hata hivyo, baada ya wananchi kushuhudia mwili huo, walikwenda nyumbani kwa mganga wa kienyeji kwa nia ya kuchoma nyumba yake moto, lakini Jeshi la Polisi lilituliza tukio hilo," alisema.

Naibu Kamishna Misime alitaja majina ya watuhumiwa hao ambao wanashikiliwa ni Seleman Nyandalu, maarufu Hango (24), mkazi Kijiji cha Chalunyangu, Saidi Msanghaa, maarufu Mangu (24), mkazi Kijiji cha Migungu na Kamba Kasubi (34), mganga wa kienyeji, mkazi wa Kijiji cha Migungu, Mtinko.

Katika tukio lingine, Naibu Kamishna Misime alisema lilitokea Dar es Salaam Agosti 19 mwaka huu; mwanamke Ezelia Kamana (36), mkazi wa Tandika Maghorofani, kudaiwa kuwa ametoweka au ametekwa.

"Jeshi la Polisi lilifungua jalada na katika uchunguzi ilibainika alikuwa na rafiki yake wa kiume, Abdallah Miraji, maarufu Musa (42), mkazi Sinza kwa Remmy, wilayani Kinondoni, ambao walikuwa na mgogoro.

Naibu Kamishna Misime alisema mwanamume huyo alikamatwa na alipohojiwa alikataa kufahamu aliko rafiki yake huyo.

Hata hivyo, Agosti 22 mwaka huu, walipokea taarifa katika Kituo cha Polisi eneo la Silversand, barabara ya Mtaa wa Freedom, Kunduchi kuwa kumeonekana mifuko ambayo ina viungo ambavyo vinadhaniwa ni vya binadamu.

"Polisi walifika eneo la tukio na kukuta mifuko minne ya viroba na katika kuichunguza, walikuta viungo ambavyo ni paja moja, vipande viwili vya mikono, eneo la kifua, makalio, 'matumbo' na nguo.

"Baada ya kupata viungo hivyo na mtuhumiwa kuelezwa, aliamua kueleza ukweli kwamba alimuua mpenzi wake na kutenganisha mwili wake katika vipande na kwenda kuvitupa maeneo tofauti," alisema.

Kamanda Misime alisema kuwa Agosti 23 mwaka huu, mtuhumiwa huyo aliongoza askari hadi eneo la Tegeta Block D na kuonesha alikotupa miguu na baadaye kuonesha alikotupa kichwa.

Katika tukio la tatu, Kamanda Misime alisema lilitokea jijini Tanga ambako mtoto Elia Elifaza (3), mkazi wa Kitongoji cha Kwedijava, wilayani Hendeni, alitoweka katika mazingira yasiyoeleweka nje ya nyumba yao tangu Agosti 19 mwaka huu.

Alisema taarifa ilitolewa polisi na uchunguzi kuanza na kukamatwa mtuhumiwa Jackson Elisante, maarufu Maeda (23), mkazi Kwedijava, eneo ambako kuna uchimbaji dhahabu.

Alisema kuwa baada ya kukamatwa na kuhojiwa, kijana huyo alikiri kumchukua mtoto huyo na kumkabidhi kwa mama yake mkubwa ambaye alikwenda naye wilayani Babati, mkoani Manyara.

"Askari waliambatana naye hadi Babati, lakini (mtuhumiwa) alibadili kauli na kueleza mtoto yupo kwa Kwedijava, wilayani Handeni, amemfukia ndani ya chumba amoishi.

"Walirejea Handeni na kuwaonesha chini ya kitanda katika chumba anamoishi alikomfukia mtoto huyo baada ya kumuua," alisema.

Naibu Kamishna Misime alitaja majina ya watuhumiwa wengine wanaoshikiliwa kutokana na tukio hilo kwa ajili ya uchunguzi ni Sadiki Lugendo, Mahiza Gumbo, Mwaligo Juma, Ali Mashaka, Juma Bakari, Abdulraman Suleiman na Bahati Daudi.

Alisema Jeshi la Polisi linatoa onyo kwa watu kuacha tabia hizo zinazotokea ndani ya jamii na kusababisha wananchi kupotea au kutekwa na matukio kuhusishwa na wivu wa mapenzi, imani za kishirikiana, tamaa za fedha au kulipiza kisasi.

Kamanda Misime alisema Jeshi la Polisi pia linatoa angalizo kwa wanaozungumzia matukio hayo, watumie majukwaa yao kwa uangalifu, kwa kuwa sababu wanazozitoa ni kutaka kubadilisha ukweli wa yanayoendelea ndani ya jamii ili kuleta taharuki na kujenga uhasama.

"Tunatoa rai kwa viongozi wa dini, wazee wa kimila wadau mbalimbali na wananchi kwa ujumla kuona matatizo haya yanayotokea ndani ya jamii, hivyo waendelee kujenga misingi bora ya kuyazuia kuanzia ngazi ya familia.

"Jeshi la Polisi lingependa kutoa onyo kali kwa baadhi ya wananachi ambao wamekuwa na tabia ya kujichukulia sheria mkononi badala ya kufuata taratibu zilizoko za kuwasilisha malalamiko ili kupata ufumbuzi kwa mujibu wa sheria.

"Wakumbuke malalamiko au kero hata siku moja hazitatuliwi kwa njia ya kujichukulia sheria mkononi, kwani kwa kufanya hivyo ni kosa kisheria ambapo husababisha madhara kwa maisha ya watu na mali zao," alisema.

Naibu Kamishna Misime alitolea mfano tukio la baadhi ya watu kujichukulia sheria mkononi ambalo lililotokea Agosti 22 mwaka huu, huko Lamadi, mkoani Simiyu la kwenda kuvamia Kituo cha Polisi na kuharibu mali.

Aliwataka wananchi wakumbuke kitendo cha aina hiyo ni kosa la jinai na kinasababisha madhara kwa binadamu, ambapo katika tukio hilo mmoja alifariki dunia, pia walizuia shughuli nyingine kuendelea.

"Tunatoa onyo wenye tabia kama hizo na yeyote mwenye mawazo ya kufanya uhalifu kama huu, Jeshi la Polisi lipo imara.

"Jeshi litachukua hatua kwa nguvu ileile ambayo watu wa aina hiyo wanatumia kutekeleza uhalifu wa kujichukulia sheria mkononi," alionya.

## HABARI KITAIFA




Katibu Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, Ado Shaibu (wa pili kulia), akizungumza wakati wa kikao cha Kamati Kuu ya chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, Othman Masoud Othman (katikati), Makamu Mwenyekiti Bara, Isihaka Mchinjita (kushoto), Kiongozi wa chama, Dorothy Semu (wa pili kushoto) na Makamu Mwenyekiti Zanzibar, Ismail Jussa. **PICHA: JOHN BADI**

# Watoza nauli kubwa kinyume cha taratibu

**Na Halfani Chusi**

NAULI ya daladala kutoka Mbagala, mkoani Dar es Salaam hadi Kimanzichana, wilayani Mkuranga, Pwani ni Sh. 3,100, lakini abiria wanatozwa Sh. 4,000, Nipashe Jumapili imebaini.

Kukiwa na nauli zilizotangazwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kila ruti, kuna maeneo ambako abiria wamekuwa wanatozwa nauli kubwa kinyume cha taratibu.

Kutokana na hali hiyo, Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Dar es Salaam, Rahim Kondo, baada ya kutafutwa na mwandishi wa habari hii kuzungumzia suala hili, alisema taarifa hizo ni ngeni kwao na kuahidi kufuatlia ili kujua ukweli.

Kwa nyakati tofauti baadhi ya abiria wa ruti ya Mbagala-Kimanzichana, akiwamo, Rashid Matimbwa, walisema kwa sasa nauli wanayolipa ni Sh. 4,000 wakati kiwango elekezi kwa ruti hiyo ni Sh. 3,100.

"Kila unapojaribu kumweleza kondakta au dereva wa daladala wanakwambia wao wanajua nauli ni Sh. 4,000, hili linaleta mkanganyiko mkubwa ukizingatia maisha ni magumu kwa ongezeko hilo la Sh. 900," alilalama Matimbwa.

Abiria mwingine, Sara Bakari, alisema kutokana na hali hiyo wamekuwa wakilipa Sh. 8,000 kila siku katika safari za kwenda na kurudi.

"Nauli kwenda Kimanzichana na kurudi Mbagala ni Sh. 8,000, ukijumlisha na fedha ya kula unajikuta umetumia fedha nyingi, hili jambo linatuumiza sisi wananchi wa chini," alilalamika Sara.

Abiria mwingine Ramadhan Msisi, alisema wameshalipigia kelele suala hilo, lakini hakuna msaada waliopata.

"Kuna mambo yanafanyika barabarani, unaweza kusema labda serikali na wamiliki wa magari wanashirikiana kwa sababu wao ndio wenye jukumu la kutatua kero hii," alisema.

Naye Mohamed Salehe alisema, "Niliwapigia LATRA ili kujua nauli halali wakamwambia ni Sh. 3,100, nilipowaeleza tunatozwa Sh. 4,000, wakasema hapana.

"Waliniambia kama kweli iko hivyo, nipande gari linalotoza nauli hiyo kisha nipige picha na tiketi zilizoandikwa bei hiyo halafu niwatumie.

"Baada ya kufanya hivyo, cha kushangaza kila nilipowapigia simu ilikuwa inatumika, ninakumbuka nilikaa sana pale Mbagala, si chini ya saa mbili, nikajua kiutu uzima wamepuuzia hoja yangu," alisema.

Mmoja wa madereva katika ruti hiyo, Juma Seif, alisema nauli wanayoitambua ni Sh. 4,000 na si Sh. 3,100 kama ambavyo abiria wanalalamika.

"Wengine hatujui bei elekezi kama ni kiasi hicho wanachosema abiria, sisi tunatoza Sh. 4,000 kwa sababu kila gari linatoza bei hiyohiyo, kama kuna bei elekezi tutakuja kuelezwa," alidai dereva huyo.

Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Dar es Salaam, Kondo, katika ufafanuzi wake, alisema, "Bado sijapokea malalamiko. Huwa tunafuatilia kila tunapopata taarifa za aina hiyo. Kwahiyo, kuhusu suala hilo nitawaagiza viongozi wa LATRA walioko pale Mbagala waanze kulifuatilia.

"Kama kuna ukiukwaji wa nauli haukubaliki, lakini hiyo taarifa nilikuwa sina, nitaifuatilia kwa kina kufahamu bei elekezi shilingi ngapi na kwanini wanatoza kiasi hicho," aliahidi.

Kondo alisema mbali na majukumu mengine, jukumu lao kubwa ni kulinda abiria na madereva na kuwaelimisha.

Alionya kitendo cha baadhi ya madereva kukatisha ruti nyakati za usiku na kupandisha nauli kiholela; atakayebainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa.

"Abiria wanapoona hayo watupe taarifa ili iwe rahisi kuchukua hatua na tunafanya hivyo katika maeneo mbalimbali.

"Abiria anapoona anatajiwa nauli kinyume cha bei elekezi, atoe taarifa bure kupitia namba 08000110019," alisema Kondo

Kondo aliwataka madereva na kondakta kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, akionya yeyote atakayebainika kwenda kinyume watamchulia hatua za kisheria.

# Biteko asisitiza TEHAMA kupewa kipaumbele

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imesema itaendelea kutoa kipaumbele katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili iwe na mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi kama inavyoelekezwa katika Dira ya Taifa ya 2025, Sera ya Maendeleo ya TEHAMA ya Mwaka 2016 na Ilani ya CCM 2020-2025.

Jijini Dar es Salaam juzi, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko aliyasema hayo wakati akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kwenye uzinduzi wa Mpango wa Ujuzi wa Kidigitali kwa Wote (DigiTrack) uliowezeshwa na Huawei na Vodacom Foundation.

Alisema serikali itaendelea kuhamasisha matumizi ya TEHAMA ili kuwezesha wananchi hususani vijana na kizazi kijacho kushindana katika uchumi wa dunia.

"Kwa kuimarisha elimu ya TEHAMA, tunajenga jamii yenye ujuzi wa kutumia teknolojia kwa ufanisi, kubuni suluhisho za ubunifu na kuchangia katika uchumi wa kidijitali.

"Hii itasaidia katika kuhakikisha kwamba maendeleo ya kidijitali yanakutanisha kila mmoja, bila kujali hali ya kiuchumi," alisema Dk Biteko.

Aliongeza serikali tafanya kila linalowezekana kuhakikisha wawekezaji wanakuwa msaada katika kubadilisha hali ya maisha ya watu kupitia nyanja mbalimbali, ikiwamo TEHAMA huku pia wawekezaji hao wakinufaika na uwekezaji wao.

Dk. Biteko alisema uchumi wa kidijiti ni muhimu katika kuleta maendeleo kwa kuongeza ufanisi katika uzalishaji na kuleta fursa na mapato ya ziada kwa wananchi.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa alipongeza Huawei na Vodacom kwa kuja na teknolojia ya Digi Truck ambayo inakwenda kuwa msaada kwa vijana wengi nchini ambayo itafika kila sehemu ili vijana wengi wajifunze.

Teknolojia hiyo iliyozinduliwa kutoka kampuni ya Vodacom Tanzania na Huawei itawezesha wananchi kupata elimu na ujuzi wa TEHAMA.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali na wadau wa TEHAMA kutoka ndani na nje ya nchi.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Pasi na kuchukua hatua mabilioni mikopo ya halmashauri yatapotea

**TAASISI** ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeokoa Sh. milioni 31.446 zilizotokana na mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani katika Halmashauri ya Mji Tunduma.

Fedha hizo zimeokolewa kutokana na ufuatiliaji uliofanywa kuanzia Juni Mosi hadi 30 mwaka huu, TAKUKURU ikikusanya kiasi hicho cha fedha kutoka vikundi maalum 20 kati ya vikundi 151 vilivyokopeshwa fedha hizo kutoka kata zote 15 za Halmashauri ya Mji Tunduma.

Uchunguzi wa taasisi hiyo umebaini kuwa kutorejeshwa mikopo hiyo ndani ya muda wa marejesho kumechangiwa na sababu mbalimbali, ikiwamo wakopaji kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu mikopo hiyo.

TAKUKURU pia imebaini sababu zingine zikijumuisha matumizi mabaya ya mikopo kwa kuwa baadhi yao hutumia fedha hizo kwenye mambo binafsi nje na dhumuni la mkopo, baadhi ya wanavikundi kukimbia na fedha za mikopo, hali ambayo imesababisha baadhi ya wanavikundi wengine kuwalipia wenzao waliokimbia, na mikopo kutolewa kwa makundi yasiyo na vigezo pamoja makundi yasiyo hai.

Upoitaja mikopo inayotolewa na halmashauri kwa makundi maalum, unarejea historia ya mikopo hiyo iliyoanzia mwaka 1993 pale serikali ilipoanzisha Mfuko wa Fedha wa Maendeleo kwa Wanawake na Vijana ili kuinua wanawake na vijana wasiojiweza kiuchumi ambao wengi wao hawakidhi vigezo vya mikopo inayotolewa na taasisi za fedha kutokana na ukosefu wa dhamana.

Kwa wakati huo, mikopo hiyo ya uwezeshaji ilitolewa asilimia tano kwa wanawake na asilimia tano kwa vijana.

Mnamo mwaka 2019, Serikali kupitia Bunge, ilirekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorejewa 2019) kwa kuongeza kifungu cha 37A mahususi kwa ajili ya kuwezesha mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Kifungu cha 37A(1) cha Sheria hiyo kinazitaka halmashauri zote kutenga asilimia 10 ya mapato yao ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyosajiliwa.

Madhumuni ya mfuko huu ni kuongeza uwezeshaji kiuchumi kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kufanya shughuli za kiuchumi ili kuboresha kiwango chao cha maisha.

Hata hivyo, licha ya dhamira hiyo njema, ufuatiliaji, ukiwamo unaofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)kila mwaka, umekuwa unabaini hatari za kutorejeshwa mabilioni yanayokopeshwa kutokana na sababu zilizotajwa hapo juu.

Mathalani, kwa mwaka 2021/22 pekee, wanufaika wa vikundi katika mamlaka 155 za serikali za mitaa hawakurejesha Sh. bilioni 47.01 kama marejesho ya mkopo, kwa mujibu wa CAG.

Mdhibiti anasema amebaini mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 178.61 ilitolewa kwa vikundi visivyokuwa na sifa na Sh. bilioni 1.24 hazikuhamishwa kutoka akaunti za amana za Mamlaka 11 za Serikali za Mitaa kwenda akaunti maalum ya mfuko, kinyume cha Kanuni ya 22 (1) na (2) ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Nipashe Jumapili tunashauri mamlaka ziwajibike kwa kutorejeshwa kwa mikopo hiyo kutokana na kutokuwa na udhibiti mzuri wa usimamizi wa mikopo.

Ili kufikia lengo na uendelevu wa mfuko, tunashauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya tathmini kabla ya kutoa mikopo na kuweka juhudi zaidi katika kukusanya madeni ambayo hayajalipwa badala ya jukumu hilo kuachwa kwa TAKUKURU.

Tunatambua kuwa kwa sasa serikali iko katika majaribio ya utaratibu mpya wa utoaji mikopo hiyo kupitia benki, lakini hatua madhubuti za kurejesha mikopo ya nyuma zichukuliwe.

Mtendaji aliyeidhinisha na atakayeidhinisha kutolewa mkopo kwa vikundi visivyo na sifa na visivyosajiliwa, awajibishwe kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi na kisheria ili kuepuka kusababisha upotevu wa mabilioni ya mfuko.

Tunaamini kuwa pasi na kuchukua hatua dhidi ya wahusika, hata utaratibu mpya wa utoaji mikopo hiyo hautakuwa na tija.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Uchaguzi Serikali za Mitaa, yaliyotokea 2019 yasijirudie

**OFISI** ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imetangaza kuwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utafanyika Novemba 27 mwaka huu.

Ni fursa muhimu kwa wananchi kuchagua viongozi watakaowaongoza katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mohamed Mchengerwa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, ndiye aliyetangaza tarehe hiyo jijini Dar es Salaam, mbele ya wadau wa siasa, wakiwamo viongozi wa vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu.

Wakati tarehe ya uchaguzi huo ikiwa imetangazwa, ni vyema pia kujikumbusha machache ambayo yalitokea katika uchaguzi wa mwaka 2019 na kusababisha baadhi ya vyama kujitoa.

Katika uchaguzi huo, vyama vinane vilijitoa kutokana na kile ambacho vyama vya upinzani vilidai kuwa ni malalamiko ya vyama kuhusu kasoro za uchaguzi huo kutofanyiwa kazi.

Malalamiko hayo yalikuwa yakielekezwa kwa chama kinachoongoza serikali, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kudaiwa kuvuruga uchaguzi huo. Kipindi hicho, Waziri aliyekuwapo, Selemani Jafo aliomba vyama vya upinzani vilegeze msimamo.

Hata hivyo, viliendelea kushikilia msimamo, vikidai kuwa wanachama wake wengi walizuia kuchukua fomu za kuwania uongozi au wale waliochukua, walizuiwa kuzirejesha baada kumaliza kuzijaza.

Katika mazingira hayo, juhudi za Jafo kutuliza upepo hazikuzaa matunda, badala yake wakaifanya CCM kushinda kwa kishindo katika uchaguzi huo uliolalamikiwa tangu mwanzo wa kuchukua fomu.

Ninaonavyo, wasimamizi wa uchaguzi watakuwa wamejifunza kitu kutoka kwenye uchaguzi wa mwaka 2019, hivyo. Ninadhani kuna haja kuhakikisha yaliyotokea wakati huo hayajirudii.

Si vibaya wale wote watakaojitokeza kuwania uongozi, wakapanda majukwaani kujinadi ili hatimaye wananchi waamue wanamchagua nani badala ya kuwapo ushindi wa mezani.

Kuwapo washindi wa bila kupingwa, kunaweza kuchangia kupatikana viongozi wasiotokana na ridhaa ya wananchi, hivyo ni vyema hilo likaepukwa katika uchaguzi ujao.

Wakati wa uchaguzi wa mwaka 2019, ilionekana wagombea wengi wa upinzani walishindwa kujaza fomu inavyotakiwa na kusababishwa waenguliwe katika kinyang'anyiro.

Kama hilo lina ukweli, basi ni vyema wagombea watakaojitokeza kuchukua fomu wawe makini ili wasiingie katika mtego uliowakumba wenzao 'waliokatwa' mwaka 2019.

Pamoja na hayo, wananchi nao hawana budi kutambua kuwa wana haki ya kuchagua au kuchaguliwa, hivyo ni muhimu wajiandae kushiriki katika uchaguzi huo, ili kupata viongozi wanaowataka.

Ninadhani si sahihi mtu mwenye sifa za kupiga kura kujiweka pembeni na kusema hataki kushiriki uchaguzi. Kujiweka pembani ni sawa na kuruhusu wachaguliwe viongozi asiowapenda.

Yapo mengi ambayo baadhi ya watu wamekuwa wakisema, ikiwamo kwamba hawataki kushiriki uchaguzi, kwa maelezo kuwa hata wakichagua, matokeo hubadilishwa na kuweka wengine.

Njia sahihi ya kuwaondoa wagombea wasiofaa ni kupigia kura wanaofaa, lakini mpigakura akikaa nyumbani, kwa maelezo kuwa hamtaki mgombea fulani, ni sawa na kumpa ushindi asiyefaa.

Hivyo, njia ya kumkataa asiyefaa, ni kujitokeza kushiriki katika kuchagua viongozi sahihi watakaoweza kutatua changamoto mbalimbali zilizomo katika jamii. Kila mwenye sifa za kupiga kura, atumie elimu ya mpigakura, ambayo hutolewa kwa wananchi wote kwa lengo la kuwawezesha kuelewa kuhusu sheria, kanuni, taratibu za mchakato mzima wa uchaguzi.

Ninaamini kupitia elimu hiyo watajua wajibu wao na umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi kwa kuwa inamwezesha mwananchi kufahamu wagombea kujua sifa za kuwa mpigakura.

Vilevile, kupitia elimu hiyo, mpigakura atakuwa anajua taratibu zinazotakiwa kufuatwa awapo katika kituo cha kupiga kura, atakuwa anajua kwanini apige kura na kwanini ampigie kura mgombea fulani.

SAFU

FIKRA MBADALA



Pascal Mayalla

# Pongezi Rais, ukweli unabaki kuwa Ngorongoro kuna tatizo

Rais Samia amepoza mtanziko wa Ngorongoro kupitia tamko la Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), William Lukuvi aliyezungumza na wananchi wa kata 11 zilizoko Tarafa ya Ngorongoro.

Waziri Lukuvi aliwasilisha maagizo ya Rais Samia aliyewatuma yeye na mawaziri wenzake kuwasilikiza wananchi hao waliokuwa wamekusanyika na kukesha kwa siku tano wakitaka kujua hatima ya malalamiko yao.

Waziri Lukuvi pia alisema Rais ameagiza uchaguzi katika tarafa hiyo kwa kutumia mipaka ya zamani, ufanyike kama unavyofanyika maeneo mengine nchini.

Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) lilianzishwa kisheria mwaka 1959 kwa Wamasai kutoka mbuga ya Serengeti kuhamishiwa Ngorongoro kama eneo la kipekee la matumizi mseto, ambako uhifadhi, utalii na maisha ya jadi ya jamii ya Wamasai vingeweza kufanyika kwa pamoja.

Lengo lilikuwa kulinda na kuhifadhi wanyamapori huku Wamasai wakiendelea na maisha yao ya ufugaji kiasili. Hata hivyo, kwa miongo kadhaa, usawa huo mwembamba kati ya makazi ya binadamu na uhifadhi wa mazingira ulianza kudhoofika.

Wamasai hao wanapewa huduma zote za afya, elimu na chakula cha kujikimu bila malipo, hali iliyopelekea Wamasai kutoka maeneo mbalimbali kujisogeza Ngorongora, ukijumlisha na kuzaliana, kukapelekea idadi ya watu ndani ya NCAA kuongezeka sana, sambamba na kuongezeka kwa idadi mifugo na kutishia ikolojia ya eneo hilo.

Idadi ya Wamasai, ambayo ilikuja mwanzo kutoka Serengeti ni takriban 8,000 mwaka 1959, sasa eneo hilo lina watu zaidi ya 100,000.

Ongezeko hili la watu limeleta mzigo mkubwa kwenye rasilimali za eneo hilo, hali iliyopelekea uharibifu wa mazingira, ulishaji mifugo kupita kiasi na migogoro kati ya uhifadhi wa wanyamapori na shughuli za binadamu.

Serikali ya Tanzania kwa kutambua hitaji muhimu la kuhifadhi ikolojia ya NCAA, ilianzisha mpango wa uhamisho wa hiari kwa jamii ya Wamasai.

Mpango huu uliratibiwa kwa kuzingatia ustawi wa Wamasai, kuhakikisha kuwa wale waliokubali kuhamia kwa hiyari, wanapatiwa ardhi ya kutosha, huduma za kisasa na msaada wa kuhamia kwenye maisha endelevu zaidi.

Uhamisho huu si wa kulazimishwa, bali ni mchakato uliyopangwa kwa uangalifu bila yeyote kushinikizwa.

Serikali imetoa ardhi mbadala za malisho, shule, vituo vya afya na huduma nyingine muhimu za jamii zikiwamo za afya na elimu katika maeneo ambako Wamasai wanapelekwa, ikiwamo Msomera.

Njia hii inalenga kuboresha hali yao ya maisha duni, wawe na maisha bora na ya kisasa, nyumba bora zenye huduma za maji na umeme huku uhifadhi wa NCAA ukiboreshwa kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Serikali imekuwa wazi kuhusu nia yake na imeendelea na mazungumzo endelevu na jamii ya Wamasai, viongozi wa eneo na wadau wengine kujibu wasiwasi wao.

Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa watu wa jamii ya Wamasai siyo tu wanahama kwa hiari kwenda katika hali bora zaidi za maisha, bali pia wanawezeshwa kustawi katika mazingira yao mapya.

Mamlaka zimekuwa makini katika jitihada zao za kuepuka aina yoyote ya ukiukwaji haki za binadamu wakati wa mchakato wa uhamisho, kuhakikisha urithi wa kitamaduni wa jamii ya Wamasai unaheshimiwa na kuhifadhiwa.

Pamoja na juhudi na nia njema za serikali, kumekuwapo na makundi mbalimbali yanasemekana kupokea fedha za nje ili kufitinisha Wamasai na wananchi dhidi ya serikali.

Kwa sasa, mchakato wa uhamisho unaendelea, huku idadi kubwa ya familia za Wamasai ikiwa imehamia maeneo mapya kwa hiari.

Serikali inaendelea kufuatilia hali hiyo kwa karibu, ikitoa msaada unaohitajika kwa wale waliohamia na kudumisha njia za wazi za mawasiliano na wale waliobaki.

Uhamisho wa Wamasai kutoka Ngorongoro ni ushahidi wa kujitolea kwa Serikali ya Tanzania kwa maendeleo endelevu, tukubali tukatae utekelezaji una mushkeli katika baadhi ya maeneo.

Kwa kuweka kipaumbele uhifadhi na ustawi wa Wamasai, serikali inafanya kazi kuhakikisha kuwa NCAA inabaki kuwa urithi wa dunia unaotambulika, huku pia ikiunda mustakabali mzuri kwa watu wa jamii ya Wamasai.

Malengo ya serikali kuhamisha Wamasai Ngorongoro ni jambo jema, lakini utekelezaji wake umekumbana na changamoto kadhaa wa kadhaa ikiwamo kutumia shinikizo kuwalazimisha waliogoma kuhama, kutaka kuwahamisha kwa kutaka kutumia nguvu kwa kuvifuta vijiji na kuzuia vyakula.

Alichofanya Rais Samia ni kutuliza tu mtanziko wa tatizo kwa kulipooza, ila tatizo bado lipo.

**Mapendekezo yangu.**

Kwanza; katika utekelezaji zoezi hili, katiba, sheria, taratibu na kanuni za uhamishaji zifuatwe.

Pili; ushirikishwa wa wahusika kwa kuwatumia viongozi wa Wamasai wenyewe kwa kuanza na ma Laigwanani wao.

Tatu; kufanya tathmini mpya ya kuwatambua Wamasai kama Indigenous people, na kufanya upembuzi yakinifu nini kina faida zaidi kati ya binadamu na wanyama, binadamu wakiwa na faida zaidi kiutalii, wanyama ndio wapishe na Tanzania tuanzishe 'indigenous people tourism' kama Marekani Red Indians, Australia Aborigines na News Zealand Maori.

Nne; jamii zote indigenous za Tanzania, wakiwamo Wahadzabe, Wamang'ati, Watindiga, Wababaig, Wabalungi na jamii asili za makabila mbalimbali zitambuliwe zilindwe na zitunzwe kama kivutio cha utalii.

Tano; kitu muhimu mamba moja kwenye taifa lolote ni watu, haiwezekani mnyama akathaminiwa kuliko binadamu, lakini binadamu akizidi kuzaliana na kutishia ikolojia, ni lazima adhibitiwe, Marekani walitumia 'Depo Provera', sisi tusifike huko.

Baada ya shari kuepushwa, ukweli unabaki Ngorongoro kuna tatizo, tutafute suluhisho la kudumu kwa kuwatendea haki kwa kutumia katiba, sheria, taratibu na kanuni.

# TAKUKURU yaokoa milioni 31/- zilizokopeshwa kwa vikundi mfu

**Na Moses Ng'wat, SONGWE**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Songwe imeokoa Sh. milioni 31.446 zilizotokana na mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani katika Halmashauri ya Mji Tunduma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kwa lengo la kutoa taarifa ya utekelezaji majukumu ya taasisi hiyo, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Songwe, Frida Wikesi, alisema ufatiliaji uliofanywa kuanzia Juni Mosi hadi 30 mwaka huu, ulifanikiwa kuokoa kiasi hicho cha fedha.

Wikesi alisema kuwa katika kipindi cha mwezi mmoja kuanzia Juni Mosi hadi 30 mwaka huu, TAKUKURU ilikusanya Sh. 31,446,000 kutoka katika vikundi maalum 20 kati ya vikundi 151 vilivyokopeshwa fedha hizo za asilimia 10 ya mapato ya ndani kutoka kata zote 15 za Halmashauri ya Mji Tunduma.

"Uchunguzi umebaini kuwa kutorejeshwa mikopo hiyo ndani ya muda wa marejesho kumechangiwa na sababu mbalimbali, ikiwamo wakopaji kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu mikopo hiyo," alisema Wikesi.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Songwe alisema sababu nyingine zilizochangia mikopo hiyo kutorejeshwa kwa wakati ni matumizi mabaya ya mikopo kwa kuwa baadhi yao hutumia fedha hizo kwenye mambo binafsi nje na dhumuni la mkopo.

"Tumebaini pia baadhi ya wanavikundi kukimbia na fedha za mikopo, hali ambayo imesababisha baadhi ya wanavikundi wengine kuwalipia wenzao waliokimbia, mikopo kutolewa kwa makundi yasiyo na vigezo pamoja makundi yasiyo hai," alifafanua zaidi Wikesi.

Alisema wamefuatilia pia utekelezaji miradi 39 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 13.412 katika sekta za elimu, maji, afya, kilimo na miundombinu.

Alisema kuwa katika ufuatiliaji huo, miradi 16 yenye thamani ya Sh. bilioni 8.249 ilibainika kuwa na upungufu kiufundi ambapo tayari ushauri umetolewa ili wahusila wafanye marekebisho.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Christina Mndeme (kushoto), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Husnuu Makame iliyopo Kibuteni, Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja juzi, alipotembelea kuona namna shule hiyo, inavyotumia mfumo wa nishati safi ya kupikia. **PICHA: OMR**

# HABARI PICHANI




Wapita njia wakipenya kwenye uzio wa vyuma ili kuvuka upande wa pili wa Barabara ya Morogoro, eneo la Mbezi Mwisho Dar es Salaam hivi kakribuni, badala ya kutumia kivuko cha daraja la juu, lililojengwa rasmi kwa ajili ya waenda kwa miguu ili kuwaepusha na ajali. **PICHA: SABATO KASIKA**



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akimpongeza Dk. Mngereza Mzee Miraji, baada ya kumuapisha kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Ikulu jijini Zanzibar jana**. PICHA: IKULU**



Madiwani wa Manispaa ya Kinondoni, wakiwa kwenye boti katika Ziwa Victoria, walipofanya ziara ya mafunzo katika Jiji la Mwanza, juzi. Katika ziara hiyo, walijifunza kuhusu ufugaji wa samaki katika vizimba ndani ya ziwa hilo, kuboresha usafi wa miji na kutembelea Daraja la J.P. Magufuli, linalounganisha Kigongo na Busisi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




Mkandarasi akiendelea na kazi ya upanuzi wa Barabara ya Morogoro, eneo la Kimara Bucha, Dar es Salaam hivi karibuni, ambapo ukikamilika, unatarajiwa kupunguza msongamano wa magari. **PICHA: SABATO KASIKA**



Wakili wa Kujitegemea, Peter Njau akizungumza na waandishi wa habari, nje ya Mahakama Kuu Kanda ya Arusha mwishoni mwa wiki, baada ya mahakama hiyo kutoa amri ya wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro kutokuhama, kutokana na tamko la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), la kufuta kata, vijiji na vitongoji vya wilaya hiyo, alilolitoa Agosti 2, mwaka huu. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

AGOSTI 25, 2024
Nipashe

# MAISHA


Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Toka hivi usiku

Ukurasa 13



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Fanya haya kupendezesha chumba chako cha kulala



Ukurasa 12

HARUSI





# Matunda zaidi ya kipodozi

Ukurasa 14

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | ■ | J | E | S | H | I |
| S | ■ | ■ | ■ | H | ■ | N |
| T | ■ | B | A | A | ■ | J |
| A | G | A | ■ | B | E | I |
| A | ■ | N | O | A | ■ | N |
| F | ■ | G | ■ | ■ | ■ | I |
| U | K | O | K | O | ■ | A |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

EDA, KUU, INA, DAU, RUNGU, IGANA, NYUKA, DAIMA, MAJESHI, UNGUZWA


## TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI



## CHEKA



Alichokifanya daktari

WATOTO wawili walikuwa wakitembea barabarani, mbele walimuona mwendesha pikipiki akihangaika kuwasha.

**Juma:** Habari kaka?

**Mwendesha pikipiki:** Safi tu.

**Juma:**Naona unaangaika na pikipiki tatizo nini?

**Mendesha pikipiki:** Napiga kiki kuwasha

**Juma:** Kwani Aziz Ki anatengeneza Honda?

**Mwendesha pikipiki:** Nyie watoto achene kunitania

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Nilijua mie bi-mdogo peke yangu kumbe tupo wengi!

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vimbwanga vya safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Bado tunajadili jinsi shetani anavyotaabisha wanawake katika kusimama kwenye nafasi ndani ya familia zao.***

Wiki iliyopita nilieleza jinsi shetani anavyotenda wanadamu kwa akili. Nikasema kuwa zipo familia ambazo shetani amepata nafasi kuzishambulia na kusababisha maumivu yasiyoelezeka.

Wiki hii, yupo dada mmoja anaishi moja ya mikoa ya kusini mwa nchi yetu, alinipigia simu kutaka ushauri. Ni baada ya kusoma kwenye mtandao moja ya makala zangu kuhusu wanawake wanavyotikisa waume zao katika ndoa.

Akasema hivi; Anti, kuna jambo linanichanganya sana, ninaomba ushauri wako. Mimi ni mke mdogo, yaani mume wangu ana mke wa kwanza ambaye wanaishi wote.

Mimi ni wa pili kanipangishia nyumba na tayari nimeshazaa naye watoto wawili, mmoja miaka tisa na mwingine miaka minne. Wote wanasoma shule nzuri. Tatizo mume wangu

> **"Mimi ni wa pili kanipangishia nyumba na tayari nimeshazaa naye watoto wawili, mmoja miaka tisa na mwingine miaka minne. Wote wanasoma shule nzuri.**

amenibadilikia, amekuwa hatusikilizani katika masuala yanayohusu familia kama awali.

Huyu bwana yupo kwenye moja ya miradi ya serikali na mimi ni mjasiriamali ninapambana kama mwanamke kuongeza pato katika familia. Lakini mwenzangu hivi sasa kanibadilikia, hanisikilizi, ananijibu mkato na matumizi ya nyumbani amekata.

Kipo kiwanja tulinunua pamoja tukaanza kujenga. Ilipofikia hatua ya kuezeka akawa hachangii tena ujenzi na hadi sasa umesimama. Kila nikimwambia tumalizie jengo ili tuhamie tuachane na nyumba ya kupanga ananijibu jeuri.

Nina kiwanja changu nilinunua mwenyewe wakati fulani nikaanza kujenga hapo nyumba. Na ujenzi huu ulitokana na fedha alizonipa wakati fulani, nikadhani amezisahau kumbe anazikumbuka.

Wakati tunazozana kuhusu ujenzi wa nyumba hii ya pamoja, akazikumbuka akaniuliza zipo wapi. Aliponibana nikamwambia nimeanzishia ujenzi kiwanja changu cha zamani kabla hatujaishi pamoja na kuzaa watoto.

Akaniambia basi uza hicho kiwanja umalizie nyumba hii ambayo inatakiwa kuezekwa na vitu vingine. Tangu aniambie hivyo, amekata mawasiliano anakuja kwangu mara moja moja na wala haachi matumizi ya watoto, bali anawalipia ada tu.

Hata hivyo, nimejitahidi tayari nimeezeka ile nyumba, nimevuta maji na bado ninaendelea kudunduliza hela kumalizia maeneo mengine ya ujenzi huu. Hayo ndiyo ninayopitia, ninaomba ushauri wako!

Msomaji wangu, bila shaka umesikia mapito ya mwenzetu. Nilijaribu kumwuliza maswali mbalimbali ikiwamo kama amewahi kudadisi nyendo za mumewe, endapo ana mwanamke mwingine huko nje baada ya yeye.

Akasema yupo rafiki yake wa karibu aliwahi kumwambia kuwa mumewe anaye mwanamke ameshazaa naye na amemjengea nyumba ambayo tayari anaishi huko. Akawa anashangaa kuwa ndio maana hamalizii nyumba yao, kumbe anamjengea mwanamke mwingine nyumba? Ama kweli Maisha ndivyo Yalivyo!

Anasema, "Siku moja ninakwenda kuwafuata wanangu shuleni, nikamwona mume wangu akiwa na mwanamke akimchukua mtoto shule ileile wanayosoma wanangu. Alipokuja nyumbani kwangu nikamwuliza, kumbe una mwanamke mwingine na mtoto?

Akaninjibu, "Ndio, tena watoto wawili kama wewe!" Nilijisikia vibaya sana, nikajua ndio maana matumizi kwangu haleti tena, wala ujenzi wa nyumba umesimama hatoi fedha anag'ang'ania niuze kiwanja changu na jengo nililoanzisha eti nimalizie nyumba.

Na mimi siuzi kiwanja changu. Pia itabidi nimwambie mama yake mzazi kuhusu jambo hili ajue kwamba mimi sipewi tena matumizi ya familia, mahaba yamehamia kwa mwanamke mwingine wa watatu!"

Msomaji wangu, mambo ndiyo hayo. Nilimpa ushauri aweze kujikwamua hapo alipo. Nawe pia tuma ushauri kwake kwa ujumbe mfupi kupitia namba mwishoni mwa makala hayo utamfikia.

Hata hivyo, kwa mtizamo wangu ninaona roho ya mitala inatesa ndugu hawa. Mwanamume ameoa mke wa kwanza ambaye anaishi naye, akatafuta mke wa kando akamweka kinyumba na kumzalisha watoto. Tena akaoa mwingine akamweka kinyumba na kumzalisha watoto.

Roho ya mitala husababisha kukosekana kwa upendo kati ya wanandoa, kutofurahia ndoa. Pia ugomvi usioisha baina ya wanandoa. Imesababisha hatma ya wengi kuharibika na ni chanzo cha ndoa nyingi kuvunjika, kuoa na kuacha na kufanya watu wawe wajane katika umri mdogo.

**Tukutane wiki ijayo kwa vimbwanga zaidi. Je, una maoni ushauri au kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581. Namba hii pia ipo WhatsApp.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Ninawakumbusha mtego kijinsia, utawaengua wanaume wengi

VITA ya kugombea madaraka imeanza kuchomoza. Wako wanaodhani tuko vibaya, wengine tuko vizuri.

Hatutumii nguvu nyingi kuangalia tunakokwenda kuliko tulikotoka. Kama nyuma pangelikuwa muhimu, labda Mwenyenzi Mungu angetuwekea macho kisogoni.

Ndiyo haikatai, ni mtazamo. Ni vita ya vyama 18, kati ya 19 vyenye usajili wa kudumu nchini, ambavyo vinajipanga kuchuana vikali.

Ni kipindi ambacho Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji umetangazwa na serikali kufanyika Novemba 27 mwaka huu, lakini uko shakani.

Kwanini? Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, akitangazia umma wa Tanzania na vyama vya siasa, kwamba Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tanzania Bara utafanyika tarehe 27 Novemba 2024.

Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), chini ya Wakili msomi Bob Wangwe na wenzake wawili wamefungua kesi kupinga mamlaka inayousimamia.

Kesi hiyo imefunguliwa Mahakama Kuu dhidi ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Wakili Bob na wenzake wanapinga uchaguzi wa serikali za vijiji, kamati za mitaa na wenyeviti wa vitongoji kusimamiwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Hilo ni takwa la kikatiba kuhoji, kutaka haki na usawa.

Wanaishtaki TAMISEMI mahakamani kwa kuwa wanaona nia yake ya kutaka kusimamia uchaguzi huo wakati kuna uamuzi wa Bunge ukielekeza Tume Huru ya Uchaguzi Tanzania (INEC) ndiyo isimamie.

Kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2019, Ibara 4 (1-3), (Tangazo la Serikali Na. 571, 572, 573 na 574) la Mwaka 2024, Waziri mwenye dhamana anayo mamlaka ya kutangazia umma na vyama vyote vya siasa tarehe rasmi ya uchaguzi.

Kwamba upigaji kura utaanza saa 12:00 asubuhi na kumalizika saa 10:00 jioni, na nafasi zitakazogombewa ni mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa halmashauri ya kijiji (kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake), wajumbe wa halmashauri ya kijiji (kundi la wanawake) na wenyeviti wa vitongoji katika mamlaka za wilaya.

Siko vizuri kwenye kupamba na kuwapendeza watu kwa hoja yangu, ambayo ninataka kuzungumza hapa, ninapojaribu kupamba mambo kwa maneno bandia, sauti yangu inafunga.

Aprili mwaka huu, Bunge lilijadili miswada mitatu ambayo inagusa mioyo ya Watanzania, demokrasia, utu na haki.

Miswada hiyo ni ule wa Sheria ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, yote ya Mwaka 2023.

Lakini yote kwa yote, kuanzishwa kosa la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji na Sheria ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023, ni hatua muhimu kwa ustawi wa jamii yetu.

Ninajua nitaamsha hisia na hasira za wengi, ambao hawakubaliani na jambo hili kwa mtazamo wa kifeministi au kwa sura ya kisiasa.

Tazama, katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji uliofanyika mwaka 2019, ni wanawake 4,171 tu, ndiyo walioshinda nafasi za wenyeviti wa vitongoji, sawa na asilimia 6.7, wanawake waliochaguliwa kuwa wenyeviti wa mitaa, walikuwa ni 528 kwa nchi nzima, sawa na asilimia 12.6; na wenyeviti wa vijiji, wanawake ni 246 tu, sawa na asilimia 2.1.

Sasa ili kudhibiti vitendo hivyo wakati wa Uchaguzi Mkuu, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ndiyo iliyokuja na hoja ya kuongeza kosa hilo, kwa kuwa vitendo hivyo vinafifisha jitihada za kitaifa kufikia usawa wa malengo ya uwiano wa 50/50 katika uongozi.

Niwakumbushe tu wanasiasa, kwamba sheria iliyotungwa hivi sasa na kutiwa saini na Rais Samia Suluhu Hassan, inakwenda kuwa mwarobaini wa tatizo hilo, na msijisahau, ni mtego kwa wanaodhalilisha wagombea wanawake.

Msisahau wenzenu, Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) walishazindua kamati ya mapambano dhidi ya ukatili wa wanawake na watoto, utakaojikita kushughulikia changamoto hizo nchini, ikiwa ni pamoja na kuandaa mwongozo utakaoshughulikia vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwenye siasa.

■ ***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI





Ni harusi ya kipekee iliyowahusisha ndugu mapacha Onesmo na Obedi baada ya kufunga ndoa na wake zao na kuandaliwa sherehe ya pamoja iliyofanyika jijini Mwanza hivi karibuni









## MITINDO

# TOKA HIVI USIKU






WATU wengi hasa vijana wanapenda kutoka usiku kwa ajili ya matembezi ya kawaida baada ya shughuli za mchana.

Hata hivyo, wengi hawajui mavazi gani yanapaswa kuvaliwa jioni hasa unapotaka kutoka kwenda kuuweka mwili sawa.

Leo nimekuletea jinsi ya kuvaa pindi unapotaka kutoka usiku.

**JEANS,SHATI NA KOTI**

Unaweza ukaamua kuvaa suruali ya jeans na shati halafu juu ukaweka na koti la kawaida kabisa, Sio lazima liwe koti la suti, ukitupia raba kali utakuwa umependeza.

**JEANS NA FULANA**

Fulana ya kubana na suruali ya jeans ni chaguo bora zaidi katika mitindo kwa vijana. Unatakiwa kuteua mitindo ya kisasa ili utakapotoka usiku utakuwa umetisha, usivae yenye michoro mingi au urembo usiokuwa na maana.

Chini tupia raba au sando nzuri katika kuboresha vazi lako.

**PANT**

Ni suruali inayotaka kufanana na 'track suits' ila yenyewe ni nzito na imeongezewa na nakshi ili iwe na muonekano mzuri/

Juu itapendeza ukivaa fulana au vesti, huku chini ukipigilia raba raba kali.

**KAPTULA**

Kaptula au pensi kama inavyojulikana na wengi huvaliwa na fulana na viatu vya simpo au viatu vya wazi.

Vazi hili humfanya mtu kujisikia huru zaidi kutokana na sehemu ya mwili kupumua kwa kuwa wazi.

UREMBO

# MATUNDA ZAIDI YA KIPODOZI

Na Mary Geofrey





WAKATI mwingine ili uweze kuboresha mwonekanao wa ngozi yako siyo lazima utumie kemikali yenye viambatano vyenye sumu.

Unaweza kutumia chakula kama matunda kwa ajili ya kusaidia kuboresha ngozi yako ya mwili ili ing'ae. Matunda hayo ni

**Parachichi**

Tunda hili lina vitamin nyingi ambapo pia huongeza mafuta mwilini kwa wale walitumialo mara kwa mara, wanashauriwa kula au kunywa juisi ya parachichi wakati wowote endapo kama huna matatazo yeyote yananahusiana na kuzidi kwa mafauta mwilini.

Pia tunda hili huongeza uzito endapo utalitumia mara kwa mara.

**Tufaa (Apple)**

Tunda hili pamoja na kupewa umaarufu mkubwa duniani na kuwa na Vitamin na madini mengi, pia lina kazi sana katika kukupa muonekano mzuri wa ngozi ya mwili wako.

Tunda hili husaidia kuboresha mzunguko wa damu pamoja na kuhifadhi ngozi isipoteze uhalisia wake.

**Ndizi**

Tunda hili husaidia kulainisha ngozi ya uso iliyokauka, kwa mfano utakuta kuna baadhi ya mafuta au losheni zimechorwa ndizi.

Kula ndizi ili urekebishe ngozi ya uso wako pamoja na kuupa uwezo mzuri wa umeng`enyaji chakula.

**Papai**

Papai pia hung'arisha ngozi rangi ya ngozi yako, yote haya hufanyika enzyme inayotokana na papai ambayo huitwa papain. Endapo kama unataka kutumia papai katika ngozi yako, basi chukua asali changanya na papai lililoiva na paka usoni kwako kwa dakika kumi kisha safisha kisha utaona kitakachotokea katika uso wako, utaonekana kama ngozi ya mtoto mchanga.



MAPISHI

# Juisi ya rozela

Na Mary Geofrey

JUISI ya rozela au choya ina wingi wa madini chuma yanayochangia uzalishaji wa damu mwilini.

Ubunifu zaidi umeongezwa katika kinywaji hiki na kwa sasa huchanganywa na matunda mengine kama nanasi, chungwa, limao, ubuyu pamoja na viungo mbalimbali.

**Jinsi ya kuandaa**

Baadhi ya watu huloweka majani ya rozela kwa muda mfupi kisha huchuja na hapo inakuwa tayari kwa kunywa lakini leo tuangazia njia nyingine ya kuchemsha.

Hatua ya kwanza ya uandaaji wa juisi ya rozela ni kuandaa jiko utakalotumia kuchemshia kinywaji hicho, kisha bandika maji kiasi kutokana na wingi wa majaini ya lozera uliyonayo kisha yaache yapate moto kidogo.

Maji yakishapata moto, weka majani ya rozela kiasi upendacho, ongeza maganda ya nanasi, tangawizi, mdalasini na iriki kama unapendelea, kisha acha yachemke.

Ili kufurahia utamu wa juisi ya rozela baadhi ya wapishi na wauzaji wa kinywaji hicho wanashauri kuchemsha kwa muda mfupi ili kuepuka juisi hiyo kukosa ladha.

Hatua inayofuata baada ya kuchemka ni kuchuja na kuongeza sukari au asali kama unapendelea na juisi yako itakuwa tayari kwa kunywa.



# DONDOO

Na Restuta James

## Fahamu mahadhi mlango mkubwa

MABADILIKO ya nyanja mbalimbali na hasa ya kiteknolojia yamerahisha upatikanaji wa taarifa hususani za kibunifu, hivyo kuongeza wigo wa maarifa kwa watu wa sekta zote.

Hii imerahisisha pia ubunifu wa ujenzi na makazi pamoja mandhari nzima ya nyumba.

Fundi seremala, Gabriel Massawe, anasema teknolojia imewasidia kuboresha kazi za ufundi kuanzia samani za ndani, mitindo ya jiko, milango, vitanda, makabati na meza za matumizi tofauti tofauti.

Akiangazia milango anagusia mikubwa ya mbele ambayo inabuniwa kwa namna ambayo inapaswa kufungwa bila kuweka mlango wa chuma (gril).

“Mwonekano wa mlango wa mbele unapaswa kuwa wa kipekee na tunashauri kama mtu anaweza aweke milango imara ya mbao za mninga au mkongo,” anasema.

Anasema milango mikubwa inaweza kunakishiwa kwa mbao na vioo ili kuleta mwonekano bora zaidi au kuacha mbao ‘iongee’ kwa kutoiwekea kitu cha nyongeza zaidi ya michoro.

Anasema kwa wapenzi wa vioo, sio lazima viwekwe kwenye milango moja kwa moja bali kinaweza kuwekwa kama mbadala wa tofali kwenye ukuta unaoshikilia mlango.

“Kama milango unayoiona (huku akionesha picha kwenye simu), mingine ni mbao plain, mingine ina maua kama hivi na wengine wanapendelea kioo, sisi tunashauri watu wasiweke magrili kwenye milango,” anasema Massawe.

Anashauri kuwa milango hasa ya kutoka nje ina nafasi kubwa katika kuboresha mwonekano wa nyumba hivyo watu wazingatie kuhakikisha ina mwonekano mzuri.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya




# Fanya haya kupendezesha chumba chako cha kulala

TUMEZOEA kujiweka safi katika uvaaji wakati wote bila kujali tuna kipato kikubwa au la.

Leo ninataka nikuambie kwamba, umaridadi huo kwenye mavazi unapawa kufanywa hata katika nyumba.

Wengi wetu tumejikuta kukikifanya chumba cha kulala kama sehemu ya kulundika vitu ovyo, eti kwa sababu hapaonekani katika uso wa wageni kama ilivyo katika sebule.

Chumba nacho kinapaswa kupangiliwa vizuri kama ilivyo kwa sebule au sehemu nyingine ya nyumba.

Kuna vitu muhimu ambavyo vinapaswa kuzingatiwa ndani ya chumba ili kukifanya kiwe chenye mvuto, chenye afya na hata kuimarisha ustawi wa nyumba yako.

Mojawapo ya vitu ambavyo vinapaswa kuzingatiwa katika kukiweka chumba chako katika hali nzuri, ni mpangilio wake hasa kwa kuangalia ukubwa na namna kilivyotengenezwa.

Zingatia kuweka vitu ambavyo ni muhimu na vina kazi na si kuweka kila kitu kwa sababu ukiweka vitu vingi ambavyo havina umuhimu kitakosa hewa na kitapoteza mvuto.


Mbali na hivo, chumba kinachokosa mpangilio mzuri, uwezekano wa kukifanyia usafi wa uhakika ni mdogo na kwa maana hiyo hatari ya kuhifadhi wadudu ni kubwa.

Hakikisha samani muhimu pekee ndio zinawekwa ndani na zinafanyiwa usafi mara kwa mara.

Kwa kitanda, zingatia kukifanyia usafi kila siku, siyo kutandika mashuka tu, lakini kuhakikisha unakikagua kila eneo na kufuta kabla ya kutandika shuka zako.

Kama kuna kabati, nalo uweke ndani yake vitu vinavyotumika pekee na kuvipangilia vizuri, ili liwe ‘smart’ na lisiharibu mpangilio wa chumba. Usiache kulisafisha kila mara.

Hakikisha nguo zako unazipangilia vizuri katika sehemu yake, na viatu sehemu yake kwa kabati lenye sehemu ya kuwekea viatu.




Kwa upande wa ‘dressing table’, kama ipo, nayo inahitaji kuwa katika mpangilio mzuri, hakikisha vitu vinavyowekwa kwayo vinakuwa katika mpangilio mzuri unaovutia. Ondoa kila kitu ambacho hakistahili kuweka hapo na uwe unalifanyia usafi kila mara.

Ukiwa na uhakika kwamba chumba chako umekifanyia usafi wa uhakika na kila kitu kimewekwa katika mpangilio mzuri, si vibaya kupuliza kwa mbali marashi ili kinukie kidogo.

Kumbuka kufungua madirisha ni muhimu ili kuingiza hewa asili na kisha kufunga baada ya kuingi hewa ya kutosha ili kuzuia wadudu kuingia.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
NILIPOFIKA NIKAKUTA MWIZI KAKAMATWA NIKAMTIA MOTO NIMEMUACHA ANAWAKA
UKIULIZWA ALIMUIBIA NANI NA ALIMUIBIA KITU GANI, SIJUI KAMA UTAJIBU!
MUDA HUO WA KUULIZA UTAUTOA WAPI BHANA?
MNAUA WAGONI MNASEMA WEZI
SASA KAMA MKEO ANA TAMAA?
MGONI NAE MWIZI KWANINI AIBE MKE WA MWENZAKE?
HIZI MADA ZINATIA HASIRA EBU KAUSHENI KWANZA
NAKUTANIA TU, NILIWAHI 'KUTOKA' NA DEMU WAKO PALE OFISINI
UTANI TU. NATOKA NA MKEO ULIHISI LAKINI NI KWELI
ANZA KUTUBU TUANZE MAISHA UPYA KABISA!
WATOTO WATANO TULIOZAA SIO WAKO WA BOSI WAKO PIA NNA MIMBA YAKE INGINE MPYA...
MERE NIMEACHANA NAE NA SIMU SIMPIGII NINA MIEZI SASA
BABA UNA-MZUNGUMZIA 'MERE MISAMBA' TULIYESHINDA KWAKE JANA?
MUAMU MBONA SIELEWI HUKU WAPI TENA?
TWENDE TUKIFIKA TUTAULIZA
BAR
'GESTI'
SHEMEJI USINIANDIKIE FAINI NIPO CHINI YA MIGUU YAKO!
NILIPOKUJA KUOA KWENU MBONA 'ULINI-PIGA FAINI SIJALALAMIKA?'

## HABARI KIMATAIFA

# Watatu wauawa katika shambulizi la kisu

**BERLIN, Ujerumani**

WATU watatu wameuawa na wengine wanne wamejeruhiwa vibaya baada ya kushambuliwa na mtu aliyejihami kwa kisu.

Shambulizi hilo limetokea jana katika tamasha la burudani lililofanyika kwenye mji wa Solingen nchini Ujerumani.

Taarifa iliyotolewa na jeshi la polisi ilisema imeanzisha msako mkali wa kumnasa mshukiwa huyo.

Msemaji wa polisi wa mji wa Dusseldorf, alisema polisi imeanzisha operesheni ya kumsaka mshukiwa, ambaye alifanikiwa kutoweka baada ya tukio hilo.

Mtu huyo huyo aliwashambulia watu kiholela akitumia kisu.

Tukio hilo lilitokea katika eneo la soko katikati ya mji huo, ambako jukwaa liliwekwa kwa ajili ya tamasha la muziki.

Tamasha hilo lilikuwa sehemu ya mfululizo wa matukio ya kusherehekea miaka 650 ya kuanzishwa mji huo.

Watu walikusanyika mjini humo kuanzia juzi jioni katika siku ya kwanza ya tamasha la siku tatu la kusherehekea kuasisiwa kwake. Zaidi ya wageni 75,000 walitarajiwa kuhudhuria sherehe hizo.

Gazeti la eneo hilo linaloitwa Solinger Tageblatt liliripoti kuwa watu watatu waliuawa na wengine tisa walikuwa katika hali mbaya.

Philipp Muller, mmoja wa waandalizi wa tamasha hilo, alisema wahudumu wa afya wanapambana kuyaokoa maisha ya watu waliojeruhiwa. Kufuatia shambulizi hilo, mji wa Solingen umezifuta sherehe hizo.

Polisi walifahamishwa kuhusu shambulizi hilo muda mfupi.

Polisi walipokuja waliwaamuru watu kuondoka katikati ya mji kufuatia shambulizi hilo.

Ilitangaza msako mkali huku vizuizi vikiwekwa katika njia zote za kuingia na kutoka katika mji huo.

Tukio hilo liliwashtusha waliokua wakihudhuria sherehe hizo. Shuhuda mmoja aliliambia gazeti la Solinger Tageblatt kuwa alikuwa amesimama mbele ya jukwaa katika eneo la Fronhof wakati shambulizi hilo lilipotokea mita chache.

Katika taarifa iliyochapishwa mtandaoni, meya wa Solingen Tim-Oliver Kurzbach, alisema mji mzima upo katika mshtuko na unaomboleza.

Mji wa Solingen una wakazi 150,000 unaopatikana umbali sawa kutoka Dusseldorf na Cologne.

Ujerumani imeshuhudia mfululizo wa mashambulizi ya visu katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, huku Waziri wa Mambo ya Ndani Nancy Faeser akiahidi kukabiliana na uhalifu wa kutumia kisu.

**DW**



Waziri Mkuu wa India Narendra Modi ,akiwa na Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, katika Ikulu ya nchi hiyo mjini Kyiv jana. **PICHA: AP**

# Modi azitaka Russia, Ukraine kuzungumza

**KYIV, Ukraine**

WAZIRI Mkuu wa India, Narendra Modi, amekutana na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, na kumtaka kufanya mazungumzo na Urusi kwa dhamira ya kumaliza vita ndani ya ardhi ya Ukraine.

Modi aliwasili nchini humo jana na kufanya mazungumzo na Zelensky akiwa na ujumbe wa amani na kuziomba nchi zote mbili kutumia meza ya mazungumzo kutafuta suluhu.

Akizungumza kwenye kikao cha pamoja na Zelensky, Modi alisema njia ya kumaliza vita ni kupitia mashauriano ya mezani na diplomasia pekee.

Alisema India iko tayari kuchukua jukumu la upatanishi utakaosaidia kupatikana amani.

Modi ambaye ni kiongozi wa kwanza wa India kuitembelea Ukraine tangu nchi hiyo ilipojitangazia uhuru kutoka Sovieti, alisema ikiwa nchi hizo mbili zitaona anatosha kuwa daraja la upatanishi, yuko tayari kutimiza wajibu huo kwa roho nyeupe.

Alimweleza Rais Zelensky kwamba India itaendelea kutoa msaada wowote wa kiutu unaohitajika wakati huu wa vita na hicho kitabakia kipaumbele cha serikali yake.

"Wakati huu wa mzozo mahitaji mengi yanaweza kujitokeza, na India imejaribu kusaidia ikiuweka mbele mtizamo wa kiutu. Ninakuhakikishia kwamba msaada wowote unaohitajika kwa msingi wa kiutu, tutakuwa nanyi na tutapambana kuwaunga mkono". alisema Modi

Hata hivyo, Zelensky hakutoa jibu kuhusu wito wa kufanya mazungumzo kutokana na kiongozi huyo kuanza kuzungumza kabla ya kumkaribisha mgeni wake.

Katika hotuba yake, Zelensky alitetea msimamo wa nchi yake wa kutaka amani chini ya misingi ya haki.

"Suala la kumaliza vita na kupatikana amani ya haki ni kipaumbele kwa Ukraine. Sisi tulifanya mkutano wetu wa kwanza wa kusaka amani. Na ningependa kuishukuru India kwa kuhudhuria. Tunatarajia India itaunga mkono maazimio ya mkutano ule." alisema Kiongozi huyo.

**DW**

# R. Kennedy Jr atangaza kumuunga mkono Trump

**WASHINGTON, Marekani**

MGOMBEA wa kujitegemea katika uchaguzi wa urais Marekani, Robert F Kennedy Jr, ametangaza kumuunga mkono mgombea wa chama cha Republican, Donald Trump.

Kennedy Jr, alijiunga katika mkutano wa kampeni uliofanyika Arizona baada ya kujiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho juzi.

Kennedy, mwenye umri wa miaka 70, alikuwa mwanachama wa Democrat kwa kipindi kirefu katika maisha yake na anatokea kwenye familia maarufu ya Kennedy.

Katika mkutano huo alisema kwamba maadili yalimfanya aondoke kwenye chama hicho sasa yamemshawishi kujitosa nyuma ya Trump na kumuunga mkono.

Katika kikao na waandishi wa habari katika mji wa Phoenix, Arizona, Kennedy alisema kwamba angeanza mchakato wa kuondoa jina lake kwenye karatasi za kura katika majimbo 10 ambayo yana ushindani mkubwa.

Hata hivyo, Trump alimsifu Kennedy na kumtaja kama mtu wa ajabu na mwerevu wakati akimkaribisha jukwaani katika eneo la Glendale.

Mpinzani wake kutoka chama cha Democrat, Kamala Harris, alisema anajaribu kupata uungwaji mkono wa wafuasi wa Kennedy.

Kennedy ni mtoto wa Seneta wa zamani wa Marekani Robert F Kennedy na ni ndugu wa rais wa zamani John F Kennedy, akitokea familia yenye ushawishi katika siasa za chama cha Democrat.

Trump aliahidi kuwa iwapo atachaguliwa tena, angefichua kwa umma nyaraka zote zilizosalia kuhusu mauaji ya rais Kennedy ya mwaka 1963.

Lakini uamuzi wa Kennedy wa kumuunga mkono mgombea wa chama cha Republican umeghadhabisha jamaa na familia yake, ambao mnamo Februari walikosoa hatua yake ya kutumia jina la familia hiyo katika tangazo katika shindano la Super Bowl.

Kerry Kennedy, ambaye ni dada yake, alisema kwamba hatua ya kumuunga mkono Trump ni kusaliti maadili ambayo baba yao na familia inachukulia kwa thamani ya kipekee.

**BBC**

## MAKALA



Na Magabilo Masambu

**Jambo la sita ni kuhusu uhakika wa bidhaa zenyewe, katika ubora, upatikanaji kudumu, maana hakuna jambo baya kwa mteja kumwambia bidhaa zimeisha, njoo siku fulani, ujue huyo ushamkosa.**

# WAZO BORA NA HATUA ZA UFANYAJI BIASHARA

BIASHARA ni maisha kwa maana nyingine maisha hayajakamilika bila kuuza na kununua. Wataalam wa fedha wanasema kama hauzi chochote, basi katika hatua za kuelekea kwenye mafanikio utazisikia kwa majirani.

Ni kweli kwamba biashara yoyote huwa inaanza na wazo, lakini wazo bora lazima liwe limekusudia kutatua changamoto za jamii. Mfano, umepata wazo la kuuza maji, maana yake unatakiwa kujua kama hilo ni tatizo katika eneo hilo.

Hivyo, jambo la kwanza kabisa unapotaka kuanzisha biashara, unatakiwa kufanya utafiti au uchunguzi mdogo kuhusiana na wazo lako la biashara. Utafiti huo ulenge kutaka kufahamu, changamoto kubwa waliyonayo wananchi wa eneo hilo. Na ikiwa utaanzisha biashara yako ni kwa kiasi gani utakwenda kutatua changamoto hiyo.

Biashara yoyote ambayo haiendi kutatua changamoto ya wakazi husika hata kama ungeifanya kwa maisha yako yote, hakuna siku utafanikiwa. Hii ni kwa sababu kama jambo ulilolanzisha si mahitaji ya watu, maana yake hutapata wateja wa kununua bidhaa zako, badala yake watafuata bidhaa ambazo ni hitaji lao.

Kupitia uchunguzi, itakuwezesha kufahamu wateja wako watakuwa kina nani. Usianzishe biashara kwa kutegemea yeyote atakayepita atanunua. Yeyote atakayepita anaweza kununua, lakini wale wateja wako uliowakusudia waendelee kuwapo.

Jambo la pili, epuka sana kuanzisha biashara inayofanywa na wengi katika eneo hilo. Unaweza kuwa unaishi mahali fulani, jirani yako anauza vitumbua na wewe ni mmoja wa wateja wake, lakini kila siku unaona wateja ni wengi sana, wazo linalokuja kichwani mwako ni kwamba 'na mimi nikianzisha hapa, nitawapata kama yeye'. Kitakachotokea kama utaanzisha maana yake mtagawana wateja, mwisho wa siku wote mtashindwa kuendelea na biashara.

Jambo la tatu, usianzishe biashara ambayo hujawahi kuifanya kwa fedha za mkopo. Siku hizi umekuja mtindo wa vikoba, kupeana fedha kila baada ya muda fulani au unaamua kwenda benki kukopa fedha kwa ajili ya biashara ambayo ni ngeni kwako.

Hakika utajuta baadaye, usifanye hivyo! Anza na mtaji mdogo ulionao. Jifunze namna unavyopata faida hata kama ni kidogo, lakini ukiweza kutunza hiyo faida ndogo na ukaweza kuikuza, basi katika biashara kubwa pia utafanya hivyo.

Jambo la nne, ni kuhusu eneo unaloanzisha biashara yako. Je, ni eneo rafiki kwa wateja wako kufika? Ndiyo maana utaona fremu nyingi ambazo ziko maeneo ya barabarani wamiliki wanatoza kodi kubwa kwa sababu wanaamini fremu ikikaa katika eneo la barabarani ni rahisi kupata wateja wale wa kudumu, pia wapita njia.

Tano, zingatia utamaduni na hali ya eneo. Bidhaa utakazouza lazima uzingatie utamaduni na hali ya eneo husika. Usifungue biashara tu kwa sababu unataka kuonekana kwamba na wewe ni mchakalikaji na kwamba wenzako wakienda kazini na wewe unakwenda kwenye biashara, unaona aibu kubaki nyumbani, bora ukae kwenye duka hata kama hakuna wateja. Mfano, unafanya biashara za makoti ya baridi Dar es Salaam, labda kama unasafirisha.

Jambo la sita ni kuhusu uhakika wa bidhaa zenyewe, katika ubora, upatikanaji kudumu, maana hakuna jambo baya kwa mteja kumwambia bidhaa zimeisha, njoo siku fulani, ujue huyo ushamkosa.

Jambo la saba, kabla ya kuanzisha biashara uwe na uhakika wa lugha utakayokuwa unaitumia kwa wateja wako, bila kujali kwamba ni wachache au watakuwa wengi kiasi gani. Watanzania wengi tulivyo, huwa biashara ikiwa mpya na tupo katika harakati za kutafuta wateja huwa tuna tumia lugha nzuri sana, lakini tukishaona wateja wamezidi tunaanza lugha za dharau, baadaye biashara zikiyumba tunaanza kiguu na njia kwa waganga wa jadi, unaanza kuona majirani zako ni wachawi, kumbe wewe mwenyewe mchawi wa biashara yako.

Mwisho ni kwenye matumizi ya fedha za biashara. Biashara nyingi zina faida kidogo na hivyo zinahitaji nidhamu ya hali ya juu katika matumizi ya fedha. Ukiwa unafanya biashara, huwezi kujua kwamba utafilisika, ni mpaka utakapofilisika, kwa sababu mtaji na faida vina tabia ya kuchanganyika.

Huwa si rahisi kujua matumizi unayofanya tayari unatumia mtaji, mpaka uishiwe, ukitaka kufanikiwa kuwa bahili, ndiyo maana wanasema matajiri wengi wana roho mbaya, lakini usiwe mchoyo, ubahili utakusaidia kulinda mtaji wako na mwisho wa siku biashara itakuwa kubwa na utakuwa na uwezo wa kuwasaidia wengi. Haya yote nimejifunza baada ya kutembelea baadhi ya wafanyabiashara mkoani Arusha, hususani katika Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru.

*0689157789*
*magabilomjalifu@gmail.com*
*Arusha-Tanzania*

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO



Na Adam Fungamwango

# 'Limbwata' inatafutwa! Hivi ipo haipo?

HIVI kweli duniani kuna dawa ya mapenzi? Kuna watu waaamini kuwa zipo dawa hasa za miti shamba ambazo zina uwezo wa kumfanya mpenzi wake ampende zaidi ya upendo wa kawaida.

Nikisema upendo zaidi ya kawaida nina maana nzito kidogo. Ni kwamba wote wanaosaka dawa za kuwapumbaza wapenzi wao mara nyingi kwanza wanaanza kupendwa. Halafu sasa wao hawataki kupendwa wanavyopendwa. Wanataka wapendwe zaidi ya wa kawaida. Yaani anayependa awe kama zezeta. Kila analoambiwa akubali. Na mara nyingi wanaopendwa wanakwenda kwa kina 'Kalumanzira' kwa ajili ya kuwapumbaza wapenzi wao wana sababu kuu mbili.

Kwanza ni kutaka udhibiti wa yeye awe peke yake, na wala mpenzi wake asiwe na hamu au kutafuta mwingine.

Pili ni uwezeshwaji. Wanachotaka kile ambacho anakipata mpenzi wake basi asilimia kubwa kama siyo 80 mpaka 90 akipate yeye. Kisiende kwa mwingine wala kisibaki kwa mpenzi wake. Ukiangalia sana hizi zote ni dalili za ubinafsi.

Ukisikiliza nyimbo nyingi zinazoimbwa, filamu na tamthili nyingi, na hata matikio mengi ya kijamii, yanaonyesha kuwa asilimia 90 au zaidi ya hapo, ambao huwa wanakwenda kwa waganga kusaka dawa za kuwapumba wapenzi wao ili wawapende zaidi ya wanavyowapenda ni wanawake.

Jamii imeipa jina dawa hiyo inaitwa 'limbwata'. Ukiutaja msamiati huo popote pale, utaambiwa kuwa ni dawa anayopewa mwanaume kwa ajili ya kudhibitiwa au 'kutiwa mikononi', asifurukute wala kutingishika.

Hapo mwanaume chochote atakachoambiwa na mpenzi wake yupo tayari, hata kile ambacho kwa wakati huo hana uwezo nacho, lakini atahangaika huku na huko hata kwa kukopa na kujitia madeni ili mradi akipeleke.

Lakini swali linakuja, hivi kweli ni lazima kutumia dawa ili kumdhibiti mpenzi? Na kweli dawa hizo zinafanya kazi?

Mpaka sasa hakuna uthibitisho wa kisayansi unaoonyesha kuwa dawa hizo za mitishamba zinafanya kazi ya kumpumbaza mpenzi zaidi ya dhana. Hata hivyo ukweli unabaki pale pale kuwa baadhi ya wanawake wanafanya hivyo.

Wanamuziki wanasemaji kuhusu 'limbwata'? Mbaraka Mwinshehe Mwaruka alitunga wimbo uitwao 'Dawa ya Mapenzi' ambao mashairi yake ni hata hapa.

"Kwa nini unahangaika kutafuta dawa ya mapenzi kwa waganga. Madawa yasiyopimwa yaweza kumuumiza mwezio we mama. Kwanza jiulize kwa nini hupendeki siku hizi mama. Bembeleza bwana yako muishi pamoja usitumie dawa.

Hakuna dawa kabisa ya mapenzi duniani, na sasa hiyo utafutayo ya kumuua mpenzi wako. Kwanza chungua na kufikiri kwa nini sasa hupendeki, uzidishapo madawa mengi, ukiachika utafanyaje?

Wengine wengi walifanya hivyo kutafuta mabwana wawapende, matokeo yalikuwa vifo na hivi sasa ni wakiwa."

Tukiachana na wimbo huo, kuna mwingine ambao ulitungwa na John Simon akiwa na JKT Kimbunga Stereo uitwao 'Ushirikina'.

"Ingawa sumu ya ugonjwa ni dawa, lakini dawa zingine mbaya, ni za kupoteza uhai. Kuna msichana mmoja hapo zamani alimpenda mumewe, akaenda kwa mganga, kutafuta dawa ya mapenzi, akamlisha mumewe.

Bwana alipokula cha jioni hakutoka nje, asubuhi na mapema watu walikuta ameshakufa.

Maisha ya mumewe sasa yameshapotea oo jama, alivyotengenea, wala haikuwa hivyo alifanya vibaya sana.

Badala ya kupendwa sasa yamekuwa majuto anahangaika. Hilo ni fundisho kwa wanawake msifanye hivyo."

Nyimbo hizi zote zinaonyesha kuwa wapo baadhi ya akinadada hao. Na zipo dawa hizo, lakini zinaonyesha kuwa badala ya kutibu tatizo, zinakwenda kuzua tatizo lingine. Nalo ni vifo kwa wapenzi wao. Kuna wanaokuwa mazezeta kabisa.

Mbaraka anakuambia hakuna kabisa dawa ya mapenzi duniani. Dawa hapa ni kujiuliza kwa nini siku hizi hupendeki. Lifanyie kazi, jibu litakuja. Hakuna binadamu duniani asiyempenda mtu anayempenda.

**"Kwa nini unahangaika kutafuta dawa ya mapenzi kwa waganga. Madawa yasiyopimwa yaweza kumuumiza mwezio we mama. Kwanza jiulize kwa nini hupendeki siku hizi mama. Bembeleza bwana yako muishi pamoja usitumie dawa.**

***Tuma meseji 0716 350534***

# HADITHI

BAADA ya kumaliza masomo yake ya kidato nne na kushindwa kuendelea na masomo kutokana na hali duni ya wazazi wake, Shani alitakiwa kuolewa. Akakubali, lakini ni kwa yule ambaye anampenda.
Haikuwa hivyo, kwani baba yake mzee Chilambo alimlazimisha aolewe na mwanamume mwenye uwezo, mali na fedha ili asiende kuteseka.
Tatizo likaanzia hapo, mwenye pesa hakupendwa na Shani, asiye na uwezo alikuwa kwenye moyo wake. Baba anamtaka mwenye uwezo. Jambo hili linazua mgogoro mkubwa kwenye familia tatu, za binti na wachumba wawili. Nini kitatokea. Usikose kila nakala ya gazeti hili.

# Aka Simtaki-8

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Kilichotokea ni kwamba baada ya kuona baba yake hataki anachokitaka, Shani alikusanya kilicho chake na kutokomea kijiji cha kijirani kiitwacho Ilembo.

Baada ya giza kuingia alilazimika kulala kwenye vichaka. Ulikuwa ni usiku mrefu sana kwake, kwani hakupata lepe la ushingizi. Pamoja na woga alionao, lakini aliona ni bora kuliwa na wanyama wakali kuliko kuendelea kukaa nyumbani kwao kwa hali ile ya kulazimishwa kuolewa na mwanaume asiyempenda.


Salum na Dora, mtu na dada yake ambao walikuwa wanakwenda shamba alfajiri ndiyo waliomuona akiwa amelala usingizu mnono alioupata alfajiri.

Kwanza walidhani ni mtu aliyekufa. Wakaogopa kumsogemea, lakini Salum alihisi anapumua, akamsongelea mpaka alipo. Alipojidhihirisha kuwa yu hai, akamwamsha.

Shani akageuza kichwa kumwangalia mtu anayemwita. Alionekana kama mtu aliyechoka mno kwa kutembea na njaa pia.

"Wewe ni nani?" Salum akauliza. "Shani!" "Shani?" "Ndiyo!" "Wa wapi, mbona kijiji hiki hakina mtu anaitwa jina hilo?" Akauliza kwa mshangao. "Natoka kijiji cha Lalangulu." Shani alikuwa akijibu kwa sauti dhaifu na yenye uchovu mkubwa. "Hiki cha jirani hapo?" "Ndiyo!" "Mbona uko hapa?" Kabla Shani kusema chochote Dora alidakia "Kaka, unamuona mtu mwenyewe hata kuongea shida, akanekana sijui kapigwa, au njaa, lakini hajiwezi huyo, hawezi kujielezea kwa sasa, ataongea kitu ambacho wakati mwingine sicho kwa sababu ya hali aliyonayo. Ninachoshauri tumchukue tumpeleka nyumbani, kama ana majeraha, au uchovu, njaa, tutajua huko huko, na akirejea hali yake ya kawaida, nadhani atatuhadhithia kila kitu."

"Sasa tunafanyaje dada na wakati tunakwenda shamba?" "Mimi nadhani tufanye hivi. Tumchukue wote wawili tumpeleke nyumbani, halafu wewe uende shambani mimi nibaki naye." Dora akadakia. Ni wazo ambalo kaka yake alilikubali bila kumwambia kitu. Akilini mwake alitambua kuwa dada yake ni mtu mwenye huruma na akili nyingi. Labda kutokana na mazingira yaliyopitia. "Ngoja nimuunue, halafu uje unisaidia tumkokote taratibu hadi nyumbani." Dora alisoge alipokuwa Shani. Akainama na kuchukua mfuko wake ulioonekana kuwa na vitu nguo chake.




**"Haya tunaona kama nitamuoa au simuoi." Akasema Fotu kwa ajili ya kutaka kuumaliza mjadala, kwani tayari kichwani mwake alishatengeneza mpango mkakati huo kabambe.**

Wakampeleka nyumbani ambako hakukuwa karibu kutoka pale kama ilivyokuwa shambani. Sehemu walipomkuta Shani kulikuwa karibu mno na shambani kwao.

Baada ya kuweka mambo sawa, Salum alianza safari yake ya kurudi alikotoka ili kuelekea shamba. Dora baada ya kumtandikia mkeka varandani aliinjika maji kwa ajili ya mgeni wake kuoga, upande mwingine akiwa anakoroga uji ili kumrudishia nguvu Shani.

***********************************

"Enhee kuna habari gani rafiki yangu?" "Habari kuhusu nini?" "Si nasikia umeshamtuma mshenga apeleke barua, majibu yameshakuja?" "Majibu yamerudi kuwa imekubaliwa, lakini kuhusu mahali na mambo mengine tusubiri kwanza kuna majadiliano yanaendelea." "Ndivyo mlivyoambiwa?" "Ndiyo?" "Wanajadiliana nini wakati wakati barua umekubaliwa?" "Si hayo niliyokwambia!" Jibu hilo lilimfanya Kibwana akaangua kicheko. "Mbona unacheka?" "Hawaambii ukweli, kuna kuna taarifa kuwa binti mwenyewe kakataa." Jibu hilo lilimshtua Fotu. "Amekataa?" "Ndiyo maana yake!" "Yule binti anikatae mimi! Ana nini, au familia yake ina kitu gani hadi anikatae mimi! Hayo majungu tu." "Sasa nani anafanya majungu?" "Kuna watu hapa hapa kijijini na hata kijijini kwa yule mwanamke, wanaeneza taarifa za uongo. Si unajua hasa kijiji hiki walikuwa wanataka sasa nimuoa Nyendo, baada ya kumuacha imekuwa nongwa. Hata wewe rafiki yangu Kibwana, siku hizi sikuamini sana." Kibwana akaangua kicheko, halafu akamtazama Fotu kwa sekunde kadhaa, halafu akasema. "Haya tupo hapa, mimi nimeambia na mtu kutoka huko huko Lalanguru na ninamuamini sana." "Ni hivi, yule binti Shani nitamuoa. Hakuna mwanamke anayekataa mwanaume mwenye pesa, tena anaolewa, anakuja kwenye familia yeye uwezo." Fotu akatamba.

"Mimi sikatai, lakini wakati mwingine rafiki yangu Fotu, mapenzi yanabebwa na hisia zaidi kuliko kitu kingine chochote. Pesa inakuja baadaye. Sikatai pesa anatakiwa, lakini baada ya kukupenda, sasa je amekupenda?" Kibwana akamuuliza Fotu. "Sina haja ya kujua hilo." Akajibu kwa kiburi. "Je mmeshawahi kukutana na kuzungumza wenyewe mkakubaliana kabla ya kupeleka posa?" "Hapana, mimi si nilikwambia nilimuona tu nilipotembea kwenye jiji chao, nikaulizia, ndiyo nikatuma posa!" "Sasa nikwambie Fotu, kwa taarifa yako, umemuacna Nyendo bure, yule msichana ana mpenzi wake anaishi kijiji hicho hicho cha Lalangulu." "Ana pesa kama mimi?" Swali hilo lilimfanya Kibwana aangue kicheko. Alipomaliza akamwambia, "sasa rafiki yangu nikuchane tu kuwa huyo kijana, jina lake simjui, hana kitu hohe hahe tu, lakini binti kafa kaoza, hasikii haambiwi. Na yeye ndiye anayesababisha binti kukataa. Nyepesi nilizopewa ni kwamba wazazi amekataa barua ya huyo kijana na kukubalia ya kwako, kwa sababu kwanza ilikuwa na pesa nyingi, halafu wameambia kuwa mtoto wa mzee Kibopa, lakini binti amepinga, anamtaka huyo huyo ambaye barua imekataliwa. Ndiyo mana ndugu yangu umewekwa kiporo. Umejibiwa lakini umeambia usubiri. Kinachofanyika sasa ni kumshawishi binti, au kumlazimisha ndicho kinachoendelea." Maneno ya Kibwana kwa mbali yalionekana kumuingia Fotu. Lakini hakutaka kuonyesha hivyo mbele ya rafiki yake huyo.

Akajimbia mwenyewe kuwa atachunguza hilo kwa njia zake. Tena hakutaka kumshirikisha rafiki yake Kibwana kwa sababu anaonekana kama yeye alipenda sana amuoe Nyendo na si Shani.

Akili yake ilimtuma kutafuta watu wengine kwa kutumia pesa za wazazi wake, kufanya uchunguzi wa kina ni kwa nini barua imekubaliwa, lakini badala ya taratibu na maandalizi ya harusi kufanyika, badala yake wanasema kuwa majadiliano? Na ni kweli kwamba binti huyo ameweka ngumu? Kuna ukweli gani kuwa kuna mwanaume kwenye kijiji hicho ambaye ni mpenzi wake? Je na yeye pia alipeleka barua? Alijibiwa vipi? Je Shani ameweka ngumu kuolewa na yeye kwa sababu ya kijana huyo au kuna kitu kingine zaidi? Je ni nani kijana huyo? Jina lake, uwezo wake na familia anayotoka. Majibu yatakayopatikana ndiyo ataamua yeye afanye nini ili kufanya chochote kitakachowezekana Shani aingine mikononi mwake.

"Haya tunaona kama nitamuoa au simuoi." Akasema Fotu kwa ajili ya kutaka kuumaliza mjadala, kwani tayari kichwani mwake alishatengeneza mpango mkakati huo kabambe.

"Sasa Nyendo ndiyo umemuacha kabisa, maana nayeye anataka kuolewa yule, akipata mchumba je?"

"Akipata aolewe, mimi akili yangu yote ipo kwa yule msichana wa Lalangulu, siyo huyu wa hapa Mtapenda."

"Mimi nina wazo moja!" "Lipi?" "Usimuache, ili dili likibuma kabisa umarudia Nyendo, nadhani ukimuomba tu msamaha anaweza kukuelewa."

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# ZARI ACHEFUKWA TENA

BAADA ya ndoa ya Zari na Shakib kuonekana kuyumba, sasa mrembo huyo ameonekana kuchefukwa na wanaume akieleza baadhi yao wana watoto wa siri.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Zari ambaye ana watoto wawili na mwanamuziki Diamond Platnumz, aliwashutumu wanaume kwa kuwa na familia za siri ambazo wapenzi wao hawazifahamu.

Hata hivyo, hakuwa wazi kama kauli hiyo inamlenga mume wake Shakib kutokana na wawili hao kuwa na mgogoro ambao unatishia uhai wa ndoa yao.

"Wanawake wanawekeza kwa siri huku wanaume wakitengeneza familia za siri," alisema Zari.

Amesema jambo hilo linawafanya wanawake na wanaume kutokuwa kwenye kiwango sawa cha kuaminiana.

## SHILOLE HATAKI YA ZAMANI

MWANAMUZIKI na mjasiriamali, Shilole, amesema watu wasitarajie kumuona kama ilivyokuwa zamani kwa sababu ameshakuwa mtu mzima.

Shilole amesema kwamba kuna baadhi ya mambo ameyapunguza ikiwamo tabia ya kuonekana kila wakati na mpenzi wake kama ilivyokuwa kwa wanaume zake wa zamani.

"Unajua ukikua unapunguza tabia zako za zamani, watu wasitarajie kuniona kila mara na mume wangu kama ilivyokuwa nyuma. Hata hivyo shemeji yenu sio mtu wa aina hiyo hapendi kuonekana," amesema.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**CHILWELL ANUKIA MAN UNITED**
KLABU ya Manchester United imepewa nafasi ya kumsajili beki wa England na klabu ya Chelsea, Ben Chilwell baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kuambiwa hayupo katika mipango ya kocha Enzo Maresca. ***(Sportsport)***

**WEST HAM YAMUWINDA SOKER**
WEST Ham inataka kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Carlos Soler mwenye umri wa miaka 27 kutoka Paris St-Germain lakini lazima wauze wachezaji kabla ya kununua. ***(Guardian)***

**BARCO KWA MKOPO SEVILLA**
MLINZI wa Brighton, Valentin Barco mwenye umri wa miaka 20 anatazamiwa kujiunga na Sevilla kwa mkopo lakini mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina haujumuishi chaguo la kumnunua. ***(Fabrizio Romano)***

**NAPOLI YASAKA NYOTA ENGLAND**
MKURUGENZI wa Napoli, Giovanni Manna amerejea England kuendelea na mazungumzo ya uhamisho wa kiungo wa kati wa Brighton na Scotland, Billy Gilmour mwenye umri wa miaka 23, mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 31, na kiungo wa kati wa Manchester United na Scotland, Scott McTominay mwenye miaka 27. ***(Gianluca di Marzio)***

**DANIEL JEBBISON AKUBALIWA**
KLABU ya Watford imekubali mkataba wa mkopo wa msimu mzima na Bournemouth kwa ajili ya mshambuliaji, Daniel Jebbison mwenye umri wa miaka 21, mzaliwa wa Canada. ***(Sky Sports)***

**JOE WORRALL HUYO FOREST**
KLABU ya Nottingham Forest imekubali ombi la kumnunua mlinzi wa England, Joe Worrall mwenye umri wa miaka 27 kutoka Burnley. ***(Football Insider)***

**STERLING ANATAKA KUBAKI**
MSHAMBULIAJI wa zamani wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 29 anataka kubakia kwenye Ligi Kuu ya England baada ya kuambiwa hana nafasi ya kuendelea kuwapo Chelsea. ***(Sky Sports)***

**BARCELONA KUMCHUKUA CHIESA**
BARCELONA wanafikiria kumnunua mshambuliaji wa Juventus na Italia, Federico Chiesa mwenye umri wa miaka 26. ***(ESPN)***

**UGARTE ANUKIA MAN UNITED**
KLABU ya Manchester United inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili kiungo wa kati wa Uruguay, Manuel Ugarte mwenye umri wa miaka 23, kutoka Paris St-Germain. ***(Sky Germany)***

**PATINO ANUKIA D'LA CORUNA**
MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Charlie Patino mwenye umri wa miaka 20, anakaribia kujiunga na Deportivo La Coruna katika uhamisho wa kudumu. ***(Athletic)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BELLINGHAM NJE MWEZI MZIMA

●●●Nyota huyo wa kimataifa wa England amebainika kuumia misuli ya....

**MADRID, Hispania**

KIUNGO wa kati wa Real Madrid, Jude Bellingham alipata jeraha la misuli ya mguu wake wa kulia mazoezini siku ya Ijumaa, klabu hiyo imethibitisha.

Chanzo kiliiambia ESPN kwamba Bellingham anatarajiwa kuwa nje ya dimba hadi katikati ya Septemba, baada ya mapumziko ya kimataifa.

Katika chapisho lake kwenye mtandao wa kijamii wa Instagram, mchezaji huyo wa kimataifa wa England alionesha kufadhaika kwa kukosa mechi na wasiwasi juu ya kazi yake baada ya msimu mgumu na Madrid na timu yake ya taifa.

“Hakuna kitu ninachochukia zaidi ya kukosa michezo lakini kujaribu kuona upande mzuri na labda mwili wangu unaniambia unahitaji ku- [redacted]

“Nimechanganyikiwa sana lakini nitakuwa nikiwaunga mkono wenzangu kama shabiki hadi niweze kuungana nao tena katika hali yangu nzuri na yenye nguvu. Asante kwa jumbe zako za wasiwasi na usaidizi. Upendo mwingi na Hala Madrid!”

Bellingham aliifungia Madrid mabao 19 ya ligi msimu uliopita, na kutoa matokeo ya mchezaji bora katika ushindi wao wa kwanza wa kombe la Ulaya na kuwashinda Atalanta katika fainali ya 'UEFA Super Cup' wiki iliyopita.

“Baada ya vipimo vilivyofanywa na huduma ya matibabu ya Real Madrid kwa mchezaji wetu Jude Bellingham, amegundulika kuwa na jeraha kwenye misuli ya mguu wa kulia,” ilisema klabu hiyo katika taarifa yake.

Madrid watacheza mechi yao ya kwanza ya nyumbani msimu huu [redacted]

kuanza kampeni kwa kutoka sare ya 1-1 ugenini dhidi ya Mallorca wikendi iliyopita.

Mchezo huo utamfanya Kylian Mbappé kucheza mechi yake ya kwanza nyumbani baada ya kujiunga na Madrid akitokea Paris Saint-Germain msimu huu wa majira ya joto.

Matarajio ni makubwa kwa Madrid msimu wa 2024-25 baada ya kumuongeza Mbappé kwenye kikosi kilichoshinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa, lakini timu ya Ancelotti ilikosolewa baada ya kuangusha pointi huko Mallorca.

“Ilikuwa wazi kabisa katika suala la tathmini,” alisema Ancelotti.

“Tulikosa usawa wakati fulani na inabidi tulifanyie kazi hilo. Sio ngumu sana. Tatizo linapokuwa wazi, kuna suluhu ya wazi.”

HABARI MICHEZO

# GREENWOOD SASA KUICHEZEA JAMAICA BADALA YA ENGLAND

**LONDON, England**



MASON Greenwood anatazamiwa kubadilisha taifa la kuichezea kutoka England na kwenda Jamaica, vyanzo vimeiambia ESPN.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 amecheza mechi moja tu ya ushindani kwa England, kama mchezaji wa akiba katika mechi ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya dhidi ya Iceland Septemba 2020.

Jamaica imefanya mbinu rasmi ya kuhamisha usajili wa kimataifa wa Greenwood na vyanzo vimeiambia ESPN kwamba mchakato unaendelea.

Greenwood aliondoka Manchester United na kujiunga na Marseille kwa mkataba wa pauni milioni 30 mwanzoni mwa msimu huu wa majira ya joto huku akitarajia kujenga upya maisha yake baada ya kushtakiwa kwa jaribio la ubakaji, kushambulia na kutumia nguvu Januari 2022.

Hata hivyo, mashtaka hayo yalitupiliwa mbali Februari 2023 na Greenwood kila mara alikanusha makosa yote.

Greenwood hakuwahi kupigwa marufuku na Shirikisho la Soka la England, FA, lakini hajashiriki kikosi hicho tangu alipocheza kwa mara ya kwanza dhidi ya Iceland.

Jamaika hivi majuzi ilimteua Steve McClaren, kocha wa zamani wa Man United kama kocha wao mpya na vyanzo vimeiambia ESPN kwamba FA ya England imeidhinisha mabadiliko hayo, na FIFA sasa imeombwa kuidhinisha ubadilishaji wa Greenwood.

# Klopp akunwa na Slot

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp alisema anaamini kuwa alama ya Arne Slot kwa Liverpool tayari iko "dhahiri," na kuongeza kuwa hakumbuki kazi hiyo, lakini anawakumbuka wachezaji.

Slot alichukua jukumu la mechi yake ya kwanza ya Ligi England Jumamosi, na kusaidia Liverpool kushinda mabao 2-0 dhidi ya Ipswich.

Ilikuwa mechi ya kwanza ya ushindani kwake baada ya Klopp, kwani Slot alichukua nafasi ya mtu ambaye alichukua jukumu la kuinoa Liverpool kwa karibu miaka tisa na kuiongoza kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019, Ligi Kuu 2020 na Kombe la FA.

Kuchukua nafasi ya kocha wa Ujerumani siku zote kungekuwa vigumu, lakini Klopp alisema alifurahi wakati Liverpool ilipogeukia kwa Slot na kuhitimisha biashara yao mapema msimu wa majira ya joto.

Katika mahojiano na ESPN Uholanzi, Klopp alisema: "Arne, ndio. Kocha mzuri sana. Nilifurahi sana niliposikia kwamba Liverpool inamchukua Arne Slot.

"Sikuhusika katika chochote, haipaswi kuwa hivyo, na mimi si mtu wa aina hiyo.

"Mambo mengi yalibadilika tangu tulipoondoka. Lakini wasiwasi pekee kwangu ulikuwa, watapata kocha mzuri?

"Liverpool walipata suluhisho la juu, la juu na la juu kwa Arne Slot."



## PSG bila Mbappe bao 10 mechi mbili

**PARIS, Ufaransa**

PARIS Saint-Germain wanaonekana kufanya vizuri bila Kylian Mbappé.

PSG iliichapa Montpellier mabao 6-0 siku ya Ijumaa na kuifanya kushinda mara mbili katika mechi mbili za ligi ya Ufaransa huku wakianza maisha bila Mbappé, ambaye amejiunga na Real Madrid msimu huu.

PSG wanatafuta taji lao la nne mfululizo la ligi lakini wengi walitarajia kushikilia kwao kombe hilo kutalegea baada ya kuondoka kwa nyota wao huyo.

Hadi sasa, hali haijawa hivyo, timu hiyo ikifunga mabao 10 katika mechi zake mbili za mwanzo.

"Kumekuwa na michezo miwili pekee lakini nimefurahishwa sana na kile nilichokiona," alisema kocha wa PSG, Luis Enrique akiiambia DAZN.

"Nina furaha sana kwa sababu ni mchezo wetu wa kwanza wa nyumbani. Tulitaka kuwapa mashabiki furaha. Ilikuwa jioni nzuri sana. Nilihisi nikiwa mazoezini, nguvu ya shinikizo iliongezeka," aliongeza.

"Tulifunga mabao sita lakini tungeweza kufunga 10. Leo (juzi) ulikuwa usiku wetu wachezaji walikuwa wa ajabu. Ni hisia kubwa."

Bradley Barcola alitangulia kufunga baada ya dakika tatu akiunganisha mpira wa kona na Marco Asensio akafunga bao la pili kwa shuti hafifu kutoka katikati ya uwanja baada ya pasi maridadi kutoka kwa João Neves.

Ilikuwa ni asisti ya tatu katika michezo miwili kwa Neves mwenye umri wa miaka 19, ambaye aliwasili kutoka Benfica msimu huu.

Pasi nzuri kabisa ya Ousmane Dembélé ikamfanya Barcola kuifunga bao rahisi la tatu dakika nane kipindi cha pili.

"Nilifurahiya sana, nilijisikia huru," alisema Barcola.

"Kocha aliomba kila mtu asonge pamoja, lazima ufanye bidii sana, lakini unazoea unapoendelea.

"Nimegundua kuwa naweza kuleta mabadiliko. Kusukuma mpira namna hiyo kwenye goli la kwanza ni jambo ambalo nimekuwa nikifanya tangu nikiwa mdogo sana."

Shuti la Achraf Hakimi lilifanya matokeo kuwa 4-0 katika dakika ya 57 na Warren Zaïre-Emery akafunga lingine katika dakika ya 20.

Mchezaji wa akiba Lee Kang-in alipata bao lake la pili katika mechi mbili alipokamilisha ushindi huo dakika nane kabla ya mchezo kumalizika.

# COASTAL UNION YAPANIA KUPINDUA MEZA KIBABE

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA msaidizi wa klabu ya Coastal Union, Ngawina Ngawina, amesema wana kila sababu ya kupindua meza kwenye mchezo wao wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravo do Maquiz ya Angola kwenye uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Katika mchezo wa kwanza uliochezwa wiki iliyopita uwanja wa Nacional da Tundwa, Angola, Coastal walikubali kipigo cha mabao 3-0 hivyo ili isonge mbele inahitaji ushindi wa angalau wa mabao 4-0.

"Matokeo yaliyopita yamepita, kwa sasa tunajipanga kwa ajili ya mchezo wetu ujao tukiwa na lengo la kupindua matokeo tuliyoyapata ugenini," alisema Ngawina.

Alisema baada ya kurudi nchini aliwapa mapumziko mafupi wachezaji wake na baadae kuanza kufanyia kazi makosa waliyoyafanya kwenye mchezo uliopita ili yasijirudie katika mchezo wa leo.

Alisema anatarajia kufanya mabadiliko kidogo kwenye kikosi kilichoanza kwenye mchezo uliopita.

"Nashukuru mpaka sasa hakuna mchezaji majeruhi, tumefanyia kazi makosa tuliyoyaona kwenye mchezo uliopita, tutapambana kuanzia dakika ya kwanza mpaka ya mwisho kuhakikisha tunapata matokeo mazuri," alisema Ngawina.

Aidha, aliwataka mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi katika mchezo huo ili kuwatia moyo wachezaji wao.

Kwa upande wake mchezaji wa timu hiyo, Jackson Shiga ambaye alizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake, alisema malengo yao ni kupindua matokeo waliyoyapata Angola.

"Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunabadilisha matokeo ambayo tuliyapata kwenye mchezo wa awali licha ya Kocha wetu Mkuu kutokuwepo, sisi haijatuathiri kwa sababu tumebaki na benchi la ufundi ambalo linafanya kazi na sisi kwa ushirikiano mkubwa, alisema Shiga.

Wakati huo huo, Msemaji wa timu hiyo Abbas El Sabri, alitoa sababu ambazo zimeufanya Uongozi wa Klabu hiyo kumuondoa aliyekuwa Kocha Mkuu, David Ouma.

Sabri, alisema sababu ambazo zimeufanya uongozi huo kumuondoa Kocha huyo ni kutoridhishwa na matokeo ambayo waliyapata kwenye mchezo wao wa awali na kwa sasa benchi la ufundi litakuwa chini ya Kocha Msaidizi Ngawina Ngawina atakayesaidiana na Joseph Lazaro.

"Uongozi umefanya maamuzi hayo baada ya kutoridhishwa na kile ambacho kilitokea tulipokuwa Angola, leo (jana), Kocha Ouma ameripoti ofisini ili wajadiliane na viongozi kwa ajili ya kupewa majukumu mengine baada ya muda mfupi tutawatangazia kile kinachoendelea juu yake," alisema El Sabri.

# Vyama vya michezo kitanzini

**Na Shufaa Lyimo**

VYAMA na mashirikisho ya michezo hapa nchini vimetakiwa kuwasilisha taarifa zao za fedha zilizopitiwa na wataalamu walioidhinishwa na Serikali kabla ya kufika Agosti 31 mwaka huu.

Hayo yalisemwa jana, na Msajili wa vyama vya michezo, Evordy Kyando wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ambapo alivitaka vyama hivyo kuwasilisha taarifa zao za fedha za miaka mitano nyuma.

"Vyama na Mashirikisho ya Michezo vimetakiwa kuwasilisha taarifa za matumizi ya fedha kwenye ofisi za Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ambazo walizitumia kwa kipindi cha miaka mitano ya nyuma kwani tunataka kuzipitia taarifa hizo," alisema Kiando.

Aidha, alisema kwa muda mrefu vyama hivyo vimekuwa haviwasilishi taarifa zao na kusisitiza wale watakaoshindwa kuwasilisha taarifa zao watafutiwa uwanachama.

"Ninaomba viongozi wa vyama hivyo wawasisitize wanachama wao, wawasilishe taarifa zao ili kuepuka adhabu ya kufutwa uanachama," alisema.

Alisema BMT imekuwa likizikagua taarifa hizo mara kwa mara ikiwa pamoja na kuangalia rasilimali ya vyama vya michezo.



Mwenyekiti wa Kamati ya maandalizi ya Selous Marathon, Imani Kajula (kulia) na Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Pwani Kaskazini, Abdul Ally, wakionesha medali zao baada ya kushiriki mbio hizo jana Mkoani Morogoro. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

## Simba yatamba kuendeleza dozi

INATOKA UK. 24

zuri na tumewekeza vizuri, wachezaji wamepata mafunzo mazuri na ni wachapakazi kweli kweli, nao wana kiu ya kupata maendeleo kwenye mchezo wa soka.

Kwa maandalizi tuliyowapa wachezaji wetu na morali waliyonayo, tuna imani tutaonyesha mpira mzuri na mashabiki watapata burudani safi," alisema kocha huyo.

Wakati Simba ikingia katika mchezo huo ikiwa na pointi tatu, ikicheza mechi moja, kwa upande wa Fountaine Gate utakuwa mchezo wao wa kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Katika hatuanyingine, Klabu ya Simba sasa rasmi watavaana na Al Ahly Tripoli ya Libya katika mchezo wa raundi ya kwanza, Kombe la Shirikisho Barani Afrika.

Hii ni baada ya juzi timu hiyo kuitandika Uhamiaji ya Zanzibar mabao 3-1 katika mchezo wa marudiano hatua ya awali uliochezwa Juni 11, Tripoli nchini Libya.

Timu hiyo imetinga raundi ya kwanza kwa jumla ya mabao 5-1, kwani katika mchezo wa mkondo wa kwanza uliochezwa Jumapili iliyopita, ilishinda mabao 2-0.

Kwa matokeo hayo, Simba itaanzia ugenini, Septemba 13 nchini Libya, kabla ya mchezo wa marudiano kuchezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Septemba 20.

## Yanga kuongeza nguvu kiungo, beki wa kati

INATOKA UK. 24

taarifa.

Hivi majuzi, Injinia Hersi alibainisha kuwa watashusha wachezaji wengine wawili kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi hicho, ingawa hakutaja maeneo watakayosajili.

"Kikosi hiki hakijakamilika, bado, nataka niwaambie tu, Yanga hii bado, tena kuna mchezaji tulitakiwa tumlete kwenye hili dirisha kubwa lakini dili halikukamilika, baada ya hapa, Januari kutakuwa na ongezeko la wachezaji wengine wawili wa kigeni. Kwa hiyo haijakamilika, ikikamilika ndiyo wanahabari tuulizeni kuhusu ubingwa wa Afrika, lakini kwa sasa bado, lengo letu ni robo fainali, tunataka tuingie makundi tuzoee kwanza makundi, halafu twende robo fainali, ila wakati mwingine Mungu huwa ana zawadi, akitupa nusu fainali, fainali au tukichukua ubingwa, sawa tutanashukuru,"

Michezo

Jumapili Agosti 25, 2024

Nipashe



Bellingham nje mwezi mzima

UKURASA 21

## Yanga kuongeza nguvu kiungo, beki wa kati

**Na Adam Fungamwango**

IMEBAINIKA kuwa klabu ya Yanga ina mpango wa kusajili kiungo mkabaji kwa ajili ya kusaidiana na Khalid Aucho na beki wa kati kubadilishana na nahodha Bakari Mwamnyeto kwenye kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Taarifa hizo zimekuja baada ya majuzi, Rais wa Klabu hiyo, Injinia Hersi Said kuweka wazi kuwa wanampango wa kusajili wachezaji wawili wa kimataifa mwezi Desemba na Januari ambako kutakuwa na kipindi cha usajili wa dirisha dogo.

Rais huyo hakutaja maeneo ambayo anatarajia kusajili, lakini habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa wanaotarajiwa kusajiliwa ni kiungo mkabaji na beki wa kati ambao watakuja kuongeza nguvu ndani ya kikosi.

Mtoa taarifa alisema kuwa atasajiliwa namba sita mwenye uzoefu wa mechi za kimataifa ili kusaidiana na Aucho, ambaye ndiye amekuwa mhimili kwa sasa na akikosekana pengo lake linaonekana.

"Akiumia au akiwa na kadi inakuwa shida sana, nakumbuka kuna michezo alikosa msimu uliopita kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika tulipata tabu, na hata ule msimu ambao tulicheza Kombe la Shirikisho Afrika mechi mbili za fainali dhidi ya USM Alger alikosekana kutokana na kadi na tuliukosa ubingwa, kwa maana hiyo tunakwenda kusajili mchezaji ambaye ana uwezo kama Aucho, au zaidi yake ili akikosekana yoyote kusiwe na pengo, Andambwile ni mzuri, lakini bado hana uzoefu sana kwenye michezo wa kimataifa," kilisema chanzo hicho.

Chanzo kimesema kuwa Yanga inahitaji pia beki wa kati wa kimataifa wa kusaidiana na Mwamnyeto, ambaye pia atamfanya Dickson Job kurejea kwenye namba za pembeni.

Yule beki 'Bacca' (Ibrahim Hamad), hana mpinzani, sasa pale tunataka Mwamnyeto na beki mwingine wawe wanabadilishana, tulimleta Gift Fred, lakini hakukidhi matarajio," alisema mtoa

INAENDELEA UK 23

# SIMBA YATAMBA KUENDELEZA DOZI

Inaivaa Fountain Gate kwenye mchezo wao wa pili wa Ligi Kuu, kimataifa sasa rasmi kuwavaa walibya huku...



**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba leo kitashuka tena Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam kucheza mchezo wa pili wa Ligi Kuu, Tanzania Bara dhidi ya Fountain Gate, huku Kocha Mkuu, Fadlu Davids, akisema wanataka kuendeleza wimbi la ushindi kama walivyofanya Jumapili iliyopita katika uwanja huo dhidi ya Tabora United.

Simba inakwenda kucheza mechi hiyo ikiwa na kumbukumbu ya kushinda mabao 3-0 katika mchezo wao kwanza wa Ligi hiyo.

Fadlu amesema hawatarajii tena kufanya makosa ya kusubiri kuwa na uhakika wa ushindi kipindi cha pili, badala yake wanataka kuimaliza mechi mapema.

"Nakumbuka mechi iliyopita hatukuimaliza kipindi cha kwanza, tukalazimika tufanye hivyo kipindi cha pili, hatutarajii tena kufanya hivyo, ila kizuri tulichokifanya katika mechi iliyopita dhidi ya Tabora United ni kulinda, hatukuruhusu wapinzani wapige shuti hata moja lililolenga lango, hili tutataka kuendelea nalo," alisema kocha huyo raia wa Afrika Kusini.

Pamoja na hayo, kocha huyo amekiri kuwa mchezo hautokuwa rahisi kwani kwa muda mfupi tu alivyowafuatilia wapinzani wake amegundua kuwa wana uwezo mkubwa wa kujilinda.

"Nafikiri Fountain Gate ni timu nzuri hasa sehemu ya ulinzi kwa jinsi nilivyoisoma kwa siku chache, kwa hiyo tumejiandaa vyema, tunakwenda kwenye mchezo huo tukiwa makini na kuheshimu wapinzani wetu.

Ni mechi ambayo naona wapinzani wetu watakaa nyuma, na sisi tutafanya kazi ya kuifungua, inatakiwa tunapopata nafasi tuitumie ili kurahisisha mchezo kwani tukipata mabao watafunguka, mchezo utaanza kuwa wa wazi," alisema Fadlu.

Kocha Mkuu wa Fountain Gate, Mohamed Muya, amesema wanaiheshimu Simba lakini hawaiogopi, hivyo wasitarajie kupata ushindi kirahisi.

"Tunaiheshimu Simba, ni timu kubwa na yenye uwekezaji mkubwa, lakini sisi ni wa-

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042